ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.

10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.
11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
34.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
41.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
42.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
43.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
44.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
45.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.

46.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
47.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
48.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
49.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
50.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
51. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
52.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
53.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
55.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
57.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
58.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
59.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
60.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
61.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
62.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
63.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
64.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
65.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.

66.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
67.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
68.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
70.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
71.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
73.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
74.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
75.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.
76.Mhe. Zahra Ali Hamad	Nafasi za Wanawake.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

BARAZA LA SABA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Kwanza – Tarehe 17 Juni, 2009

Kikao kilianza saa 3: 00 asubuhi

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

KIAPO CHA UAMINIFU

Mheshimiwa afuatae aliapa kiapo cha uaminifu na kukaa katika nafasi yake ndani ya Baraza.

Mhe. Asha Moh'd Hilal:

Mhe. Spika: Mhe. Asha Moh'd Hilal karibu sana katika shughuli zetu, chukua nafasi upande wa mkono wa kulia. (*Kicheko*)

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe, naona Mhe. Asha kapata nafasi baada ya kukaribishwa na Mhe. Ali Suleiman Ali. Ahsante sana.

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza karibuni tena katika shughuli zetu za mkutano huu wa Bajeti ambao unaanza leo. Tunamshukuru mwenzetu aliyechaguliwa na ameshaapishwa rasmi na yuko tayari sasa kwa ajili ya kuendelea na shughuli zetu za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Asha Moh'd Hilal karibu sana katika shughuli zetu, huko uliko ndio upande wa chama kinachotawala na upande wa kushoto yangu ni upande wa chama cha upinzani. Kiutaratibu katika shughuli zetu huwa tunafanya kazi pamoja, karibu sana.

Waheshimiwa Wajumbe, kifungu cha 71(2) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kinaeleza kwamba Spika wa Baraza la Wawakilishi atatoa taarifa rasmi kwa Baraza na kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar kuhusu kiti cha Mjumbe Mwakilishi kuwa wazi katika kutekeleza masharti ya kifungu cha

kwanza cha kifungu hiki. Aidha kifungu cha 6(4) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2007 kinaelezea ifuatavyo:-
"Spika atatangaza katika Baraza kuhusu kifo cha Mjumbe yeyote kinapotokea na pia atatoa taarifa ya kifo hicho kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi au Rais kwa kadiri itakavyokuwa kuwa kiti cha Mjumbe aliyefariki kiwazi".

Waheshimiwa Wajumbe kwa kutekeleza matakwa na maelekezo ya vifungu hivyo vya Katiba na Kanuni nilivyovinukuu hapo awali na kwa huzuni na masikitiko makubwa, natangaza mbele ya Baraza hili kwamba Mhe. Soud Yussuf Mgeni aliyekuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Jimbo la Wawi la Pemba amefariki dunia.

Mhe. Soud Yussuf alifariki dunia siku ya Ijumaa tarehe 22 Mei, 2009 huko Dar es Salaam katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Alizikwa huko kijijini kwao Ng'ambwa Pemba siku ya Jumamosi tarehe 23 Mei, 2009. Kwa hivyo, kiti cha Mjumbe Mwakilishi wa Jimbo la Wawi kiko wazi kuanzia tarehe hiyo aliyofariki.

Vile vile ninawaarifu kwamba tayari nimeshatoa taarifa rasmi kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa mujibu wa kifungu hicho cha 71(2) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 toleo la 2003 kuwa kiti cha Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi Jimbo la Wawi kiko wazi kuanzia tarehe 22 Mei, 2009 kutokana na kifo cha Mhe. Soud aliyekuwa Mjumbe Mwakilishi wa jimbo hilo.

Naomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Baraza letu hili la Wawakilishi la Zanzibar, kutoa mkono wa pole kwa familia ya marehemu, ndugu, jamaa, marafiki na wananchi wa Jimbo la Wawi na kwa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuondokewa na kipenzi chetu, mwenzetu huyu, marehemu Mhe. Soud Yussuf Mgeni. Sote kwa pamoja tumuombe Mwenyezi Mungu atupe moyo wa subira na tumuombe amlaze mahala pema peponi AMIN.

Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kutokana na taarifa hii nikuombeni tusimame kwa dakika moja kumkumbuka mwenzetu.

Waheshimiwa Wajumbe walisimama kwa dakika moja kumkumbuka Marehemu Mhe. Soud Yussuf Mgeni

Mhe. Spika: Ahsanteni sana.

Mheshimiwa mwenzetu huyu ambaye tumemuombea dua hivi sasa, yeye alikuwa ni *chief weep* kwa upande wa upinzani. Wenzetu wa upande wa

upinzani tayari wamefanya kikao chao na kumteuwa Mhe. Haji Faki Shaali kuwa *chief weep* mpya wa upande huo. (*Makofi*)

Naomba kutoa taarifa hiyo na naomba sasa anyanyuke ili mumuelewe. Anaanza kazi yake rasmi katika Baraza hili leo hii.

Waheshimiwa Wajumbe, kutokana na taarifa ambayo Mhe. Mwenyekiti wa Tume nimemuarifu juu ya kifo hiki na jimbo hilo kuwa wazi, nimepokea barua kutoka kwa Mwenyekiti huyo kwamba jimbo hilo kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi litaendelea kuwa wazi na litajazwa wakati wa uchaguzi mkuu. Nakushukuruni kwa taarifa hiyo.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi (Kny: Mhe. Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri Kiongozi naomba kuwasilisha mezani nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 9 April, 2009.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2009/2010.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 102

Mfuko wa Marais JK na AK

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza:-

Azma ya serikali zetu mbili ya Muungano na ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwapunguzia umasikini wananchi wake kwa kubuni mpango “MKUZA” kwa Zanzibar na “MKUKUTA” kwa Tanzania Bara. Pia Marais wetu hawa wametoa fedha nyingi ili kuwasaidia wananchi wake kupambana na ukali wa maisha.

(a) Je, Mhe. Waziri tangu kuanza kwa huduma ya Mfuko huu wa Marais wetu JK na AK tumepata mafanikio gani.

(b) Ni kiasi gani cha fedha kimetolewa hapa Zanzibar tangu kuanza kutolewa kwa fedha za Mifuko hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi (Kny: Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto) – Alijibu:-

Mhe. Spika: Mhe. Waziri leo amekuwa *spare part* yetu kubwa. *(Kicheko)*

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kazi, Maendelezo ya Vijana, Wanawake na Watoto naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suwali lake Nam. 102 lenye vifungu a na b kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza nakubaliana kabisa na Mhe. ALi Abdalla kwamba, kwa nia njema tu marais wetu hawa wawili wametoa fedha nyingi ili kuwasaidia wananchi wake kupambana na ukali wa maisha. Nitajibu swali lake a na b kwa pamoja.

(A) Tangu kuanza kwa huduma ya mfuko huu wa Marais wetu Mhe. Jakaya Mrisho na Mhe. Amani Abeid Karume kwa kiwango fulani tumepata mafanikio makubwa.

(B) tokea kuanzishwa kwa mfuko huu, takriban shilingi zipatazo milioni mia tatu na hamsini zimeshatolewa hadi hivi sasa kwa mikoa yote ya unguja na pemba.

(C) Mhe. Spika, lazima tukiri, ni kweli kwamba fedha zilizowekwa ni nyingi kuliko zilizotolewa, lakini haya yametokana na matatizo ya kiutendaji. Mhe. spika, unavyopanga kutekeleza hasa mambo ya mkopo tulikuwa na matatizo kwanza kwenye ujazaji wa fomu, pili kuwahamasisha wananchi wenyewe kuhusu hili suala la fomu.

Nitatoa mfano, tumepokea maombi mengi sana ya wananchi, kwa mfano mtu ana biashara ndogo ndogo labda ya maandazi au samaki, anakwenda kukopa shilingi milioni 15. sasa matatizo kama hayo ni mengi na utakuta watu wa benki kwa vile pesa hizi lazima zifuate masharti ya benki basi mtu yule hana dhamana. Kwa hivyo matatizo kama hayo ndiyo yaliyotokea na mengine ya ujazaji wa fomu, ndio maana kidiogo jamaa wakawa waangalifu katika utoaji wa mikopo hii.

sasa tunashukuru awamu ya kwanza hii imetolewa na fedha nyingi hizi zimetoka Mkoa wa Mjini Magharibi ambapo wao zaidi ya milioni 200 zimetolewa, lakini kwa kweli tunaendelea katika Mikoa mingine na hasa

kazi kubwa ni kuwaelimisha wananchi, tunataka kuondoa ile dhana kwamba fedha hizi zimetolewa halafu watu wasizilipe, ninachotaka wazilipe kwa mujibu wa uwezo wa mtu, hiyo ndio dhana kubwa na ndio maana utaona kwamba kasi yake ya utoaji ni ndogo.

Mhe. spika, naomba kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba makosa tumeyaona, tumeshakaa na sasa tunajipanga vizuri kati ya serikali za wilaya, Mikoa na wizara yenyewe pamoja na benki kufanikisha vyema suala hili.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsane sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Kaimu Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Amesema kwamba mafanikio makubwa yamepatikana katika kutoa fedha hizi za zilizotoka kwa JK na AK na amesema Mkoa wa Mjini Magharibi ndio uliopata fedha nyingi.

Je, anaweza kunitajia katika wilaya zilizobakia? Kwa sababu Zanzibar ina wilaya 10, anaweza kutwambia kwa kila wilaya zilizobakia watapata kiasi gani.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi (Kny: Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto): Mhe. Spika, kwa kweli sina hizo *figure* kwa hivi sasa, lakini naomba kwa ruhusa yako Mhe. Spika, madhali vikao vinaendelea nitamtafutia hii leo na kesho nitakuja na jawabu rasmi ya pesa kamili zilizotolewa au Jumatatu tukijaaliwa.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa majibu ya Mhe. Waziri inaonekana kwamba suala zima lililokusudiwa kuhusiana na fedha hizi halikwenda vizuri kwa sababu pesa iliyotolewa ni ndogo kuliko ile iliyokuwa haijatolewa.

Ikiwa hivyo ndivyo na kutokana na majibu yake kwamba kuna tatizo namna ya kulipa na uwezo wa yule mtu anayetakiwa kulipa. Sasa katika suala hili hili la MKUZA na MKUKUTA

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi (Kny: Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto): Mhe. Spika, ni kweli ahadi hiyo Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano aliitoa, lakini ukichukulia ajira milioni moja haikusudiwi ajira ya serikalini, *Private*

Sector ni ajira, kukaanga samaki, kufanya biashara ndogo ndogo ni ajira unajiajiri mwenyewe. Muhimu kwamba serikali itawawezesha hilo ndilo suala la msingi kuwasaidia kujikwamua huo aliouzungumza Mheshimiwa umasikini.

Suala la msingi ni kujikwamua na umasikini na hiyo ajira wewe ukiweza kujiajiri mwenyewe sisi tunahesabu basi *your leased pendent.*

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Kaimu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, bahati nzuri Mfuko huu upo katika Kamati yangu ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Tegemeo letu kubwa tangu zilipotoka fedha hizi basi labda tuna mzunguko wa tatu kutolewa ili wananchi wetu wafaidike.

Kwa kuwa Wizara ya Fedha na Uchumi pamoja na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kupitia benki zetu walitoa taaluma mbali mbali kwa wananchi kabla ya kutoa fedha hizi. Kwa taarifa niliyonayo kuna eneo la Shehia ya Matemwe walikwenda kutoa mafunzo ya watu 50 na katika hao katokea mmoja tu aliyefaulu.

Je, hawa wataalamu wetu kweli wana nia njema ya kuwaelewesha watu na wakaelewa ili kupata fedha hizo kutumia kwa maisha yao na kusaidia wengine.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi (Kny: Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto): Mhe. Spika, ni kweli tunakubali kuna matatizo yamejitokeza kwenye utendaji kama nilivyosema kwenye jawabu langu la msingi.

Hili suala alilolizungumza la Shehia ya Matemwe ni kweli limetokezea. Nataka kusisitiza kwamba kama alivyozungumza Mhe. Ali Suleiman kwamba suala la elimu ni suala la msingi, mbali ya Shehia ya Matemwe lakini tutajitahidi kupangana vizuri sasa twende karibu katika wilaya zote kuwaelimisha wananchi juu ya azma nzima ya Mfuko huu na taratibu zake.

Tumehisi kwamba kidogo uelewa watu hawakuufahamu vizuri, kwa kweli fedha zipo lakini hizi ni za mkopo na unapotaka kukopa lazima ujitizame mwenyewe uwezo wako wa kulipa. Sasa hapa ndipo palipokuwa na matatizo kidogo. Kwa hivyo, tunajipanga vizuri tutarudi tena Shehia ya Matemwe, nakuhakikishia Mhe. Ali Suleiman na Mhe. Ame Mati Wadi kwamba tutaungana nay eye na Mhe. Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa

tutarudi kule tutaweka sawa mambo haya ili tufaidike sote na Mfuko huu. Ahsante.

Nam. 20

Usajili wa Mali

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:-

Serikali kupitia Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, kwa nia njema kabisa, imeanzisha zoezi la usajili wa mashamba na nyumba, kwa watu wanaomiliki mali hizo katika nchi yetu.

Mhe. Waziri, kwa kuwa katika Idara hii, kuna baadhi ya wafanyakazi, hudai rushwa ili mwananchi atimiziwe kazi yake haraka. Je, ni hatua gani za kinidhamu zitachukuliwa kwa watendaji watakaobainika kuchukua rushwa katika zoezi hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swala lake Nam. 20 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli Wizara yangu ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kupitia Idara zake za masuala ya Ardhi zimo katika utaratibu wa zoezi la Usajili wa Ardhi na mali zilizoambatana nazo kuweka sawa kumbukumbu za haki za matumizi kwa wenye haki hizo katika nchi yetu.

Zoezi hili ni la muhimu kwa manufaa na maendeleo na matumizi mbali mbali kwa wananchi hao. Hivyo kukwamisha zoezi hili kwa njia yoyote ni kwenda kinyume na utaratibu na ni kuvunja Sheria ya Usajili wa Ardhi. Pia kudai rushwa ni kosa la jinai ikibainika kwamba kuna mfanyakazi amefanya kosa hilo la kudai rushwa katika zoezi la usajili wa ardhi, hatua za Kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Mhe. Spika, Aidha, vyombo vya Kisheria vitakapothibitisha kutendeka kwa kosa hilo na mfanyakazi huyo na kupewa adhabu inayostahiki na Mahkama basi pia atakuwa amejifukuzisha kazi mwenyewe.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwamba kosa lolote la rushwa ni kosa na mtoaji au mpokeaji rushwa huwa ni adui wa nchi au haki ya maendeleo katika nchi yetu,

Je, kwa kuwa baadhi ya watu walalamikaji wapo na wanatujia sisi, huo utakuwa ni uthibitisho wa kwanza kwa kuwa katoka kwake kanijia mimi ana kitu cha uhakika, akibainisha mtu fulani wizara pamoja na kueleza maelezo haya aletwe ili atoe ushahidi mbele yao Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, wizara yangu Mhe. Waziri, mimi na watendaji wote tuko pale kwa ajili ya wananchi. Endapo kuna mwananchi yeyote amekwenda kwa Mwakilishi yeyote kupeleka madai yake, ningemuomba Mwakilishi afuatane na mtu huyo aje afisini kwangu siku yoyote, saa moja na robo asubuhi, siku yoyote ile.

Nam. 12

Kocha wa Riadha

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Naipongeza Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa kuleta kocha wa mpira wa miguu kutoka Misri na kupitia kocha huyo hupata nafasi ya kwenda Misri kufanya mazoezi na michezo ya majaribio.

(a) Je, Mhe. Waziri ni lini Serikali itatupatia kocha wa riadha ili kunyanyuwa vipaji vya wanariadha wetu na kuufanya mchezo huo uwe tegemeo zaidi kwa kutupatia ushindi Kitaifa na Kimataifa.

(b) Je, Serikali hutoa msaada gani kwa wanariadha wetu wanaposhiriki mashindano ya Kimataifa wakipeperusha Bendera ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote kuwepo hapa tukiwa wazima.

Mhe. Spika, sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 12 lenye vifungu a na b kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, tayari Serikali kupitia Wizara yangu imeshachukua hatua ya kupata mwalimu (Kocha) wa riadha wa kuwasaidia wanariadha wetu kunyanyua vipaji vyao na pia kuviendeleza hadi kufikia viwango vya juu ili kutuwakilisha vizuri kwenye michezo ya Kitaifa na Kimataifa.

Mhe. Spika, Serikali kutokana na uhusiano wake mzuri na Serikali ya Cuba, nchi hiyo tayari imeshakubali ombi letu la kutupatia Kocha wa riadha na tayari Ubalozi wa Cuba nchini Tanzania umeshatuletea taarifa rasmi juu ya Kocha huyo na Wataalamu wetu wa mchezo wa riadha wameridhika na sifa zake.

Mhe. Spika, Kocha wa riadha kutoka Cuba alikuwa awasili hapa nchini mwezi wa Januari, 2009 lakini kutoakana na matengenezo ya Kiwanja cha Amaan ambacho ndicho kiwanja kikuu kilichothibitishwa na ndicho kikuu kwa shughuli za mazoezi ya riadha na ambacho kilikuwa kitumike kwa mafunzo ya wanariadha wetu wa hapa nchini chini ya Kocha kutoka Cuba haikuwezekana kumleta kutokana na matengenezo yanayofanyika katika uwanja huo. Hivyo, Serikali imeuomba Ubalozi wa cuba kucheleweshe kuwasili kwa Kocha huyo hadi yatapomalizika matengenezo ya kiwanja ambacho hivi sasa yanaendelea vizuri.

(b) Mhe. Spika, Serikali inatoa misaada mingi kwa wanariadha wetu ili kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye mashindano yote ambayo wanashiriki. hususan pale wanapopeperusha bendera ya zanzibar.

Mhe. Spika, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar huwapatia wanariadha wetu fedha za kujikimu, usafiri, malazi na chakula kila wanaposhiriki kuiwakilisha Zanzibar kwenye mashindano ya Kitaifa na Kimataifa na kila pale ambapo uwezo wa ziada unaruhusu.

Mhe. Spika, mfano mzuri ni wa hivi karibuni ambapo wanariadha wanne tayari wamepatiwa teketi 4 na Baraza la Michezo Zanzibar ili kuwawezesha kushiriki katika mashindano ya **msitu – wa – nyika** huko Moroko, bila ya msaada huo wa Serikali kwa chama cha riadha na wana riadha hao wa Zanzibar basi hayo yasingeweza kufanyika.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba ruhusa kuuliza swali moja la nyongeza. Tunaipongeza serikali kwa juhudi za kutafuta mwalimu wa riadha ili wakimbiaji wetu wapate viwango ili waweze kushindana kimataifa. Katika kujibu swali Mhe. Niabu Waziri amesema kuwa taaluma hiyo ataifanyia Kiwancha cha Amani ambacho ndicho kitachokuwa na kiwango cha kufundishia.

Je, sisi tunaoishi vijijini utaratibu gani ametuwekea ili vijana wetu waweze kufika Amani kupata mafunzo kutoka kwa mwalimu huyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, naomba nimthibitishie kwamba Chama cha Riadha Zanzibar kimejipangia utaratibu wake maalum, yaani programu maalum ambayo wanazunguka kisiwani Unguja na Pemba katika kila sehemu ambapo kuna mambo ya riadha yanaendelea, pia wanazunguka katika skuli zetu kuibua vipaji mbali mbali vya riadha.

Baada ya wao kuibua vipaji hivyo huwachukua wale wachezaji na kuwaweka kwenye kambi maalum ili kuwafunza waweze kufikia kiwango cha kitaifa na kimataifa. Kwa hivyo, hilo linafanyika chini ya Chama cha Riadha cha Zanzibar bila ya utaalam wa kocha huyo. Kocha huyo anapokuja huwa anashughulikia zaidi Timu ya Taifa na vile vipaji ambavyo tayari vimeshapatikana ili visukwe kuweza kutuwakilisha Zanzibar kimataifa.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa kiwango ni kidogo cha mpira wa mikono hapa Zanzibar, na kwa kuwa makocha wengi huelekezwa katika mpira wa miguu na riadha. Je, Mhe. Waziri ni lini utatupatia makocha wa wanawake hapa Zanzibar.

Mhe. Spika: Saidia hili swali ili tuweke mambo sawa. Lazima *gender sensitivity* iangaliwe.

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, swali la Mhe. Mwakilishi ni zuri sana na limekuja kwa wakati muafaka. Nafikiri baada ya wiki mbili zijazo kuna makocha wawili kutoka Afrika Kusini watakuja kupiga kambi hapa Zanzibar kwa mwezi mmoja kuwafundisha kinamama wa *netball*.

Lakini katika hiyo hiyo riadha iliyozungumzwa na Naibu Waziri makocha hao pia kwa sababu wamo kinamama wanaofanya riadha na wao watakuwa *definately* wamehusishwa.

Kwa hivyo, katika masuala haya hatuhusiki na *gender* lakini wote kinamama na kinababa alimuradi wanafikia viwango vya kufundishwa. Wale ambao hawafikii kuna programu maalum ya vijijini itakayosimamiwa na *university* ya Indiana iko njiani wanakuja kwa vijiji vyote Unguja na Pemba. Tutashirikisha vijana wa riadha, *football*, *basketball* na *volleyball* Pemba na Unguja wanawake na wanaume.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika miezi miwili ijayo kutakuwa na mashindano ya riadha kwa Tanzania

nzima kitaifa na mikoa yetu imetakiwa ishiriki kikamilifu kupeleka wanariadha. Kwa kuwa ofisi zetu za mikoa hazina uwezo je, wizara itatusaidia vipi ili kuweza kusafirisha wanariadha hao. Hasa ikizingatiwa kwamba katika riadha ya mwaka jana Mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa wa kwanza kwa Tanzania na Mkoa wa Kusini tulikuwa wa tatu kwa Tanzania.

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, bajeti ya Idara ya Michezo tumeipitisha katika Baraza hili na michezo iko mingi ikijumlisha na hiyo ya riadha. Tumetoa wito kwa Wakuu wa Mikoa, vyama vya siasa kusaidia inapotokea hoja kama hizi, kama ni kuchangisha au kutafuta aina yoyote ya mifuko kutafuta wafadhili, ili hawa wanaohusika waweze kushiriki.

Kwa kutegemea mfuko wa idara yangu peke yake kwa mikoa yote mitano ya Zanzibar, hiyo itakuwa ni vigumu kabisa kuweza kuwahudumia hao wanariadha watakaoteuliwa kushiriki. Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wote tushirikiane kutafuta nyenzo za kupata fedha za kuwapeleka hao watakaoteuliwa.

Nam. 29

Huduma ya Upokeaji wa Dawa, Katika Dirisha la Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Ali Denge Makame - Aliuliza:-

Kwa kuwa kuna usumbufu mkubwa katika sehemu ya kutolewa dawa (sehemu ya dirishani) Hospitali ya Mnazimmoja.

(a) Je, Mhe. Waziri, Wizara yako imejipanga vipi ili kuhakikisha kwamba usumbufu uliopo unaondoka.

(b) Je, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba, wagonjwa wanaopokea dawa dirishani hapo, hawapewi maelekezo mazuri ya matumizi sahihi ya dawa hizo, jambo ambalo ni hatari kwa wagonjwa husika.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 29 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa kuna usumbufu mkubwa hasa wakati wa zamu za asubuhi sehemu ya kutoela dawa dirishani katika Hospitali ya Mnazi Mmoja unaotokana na msongomano wa wagonjwa.

(a) Mhe. Spika, ili kuhakikisha kwamba usumbufu uliopo unaondoka Wizara yangu inaendelea kuimarisha huduma za Afya katika Hospitali za Wilaya na Vijini Unguja na Pemba ili viweze kutoa huduma za uzazi na motto, meno na kadhalika. Sambamba na haya Wizara pia inaendelea kufundisha Wauguzi, Madaktari Wasaidizi, Wafanyakazi wa Maabara na Wahudumu wengine kwa lengo la kupunguza msongomano katika Hospitali ya Mnazo Mmoja pamoja na kuwapunguzia wananchi adha ya kusafiri masafa marefu ya kutafuta huduma.

(b) Mhe. Spika, siyo sahihi kwamba wagonjwa wanaopokea dawa dirishani hawapewi maelezo mazuri ya matumizi ya dawa hizo. Wagonjwa wote wanaopata dawa dirishani huwa wanapewa maelekezo jinsi ya kutumia dawa. Ikumbukwe kuwa dawa ni kemikali ambazo kama hazikutolewa maelekezo mazuri zinaweza kuwa na athari, hivyo wafamasia wetu huwa wanatoa maelekezo ya ana kwa ana pamoja na maandishi kila wanapotoa dawa kwa wagonjwa.

Mhe. Spika, naomba kutoa wito kwa wananchi wote kuwa wasisite kuuliza maswali kwa mafamasia juu ya dawa wanazopewa iwapo hawakufahamu vizuri maelekezo waliyopewa.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa asubuhi ya leo na mimi kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Waziri anakubali kwamba yapo mapungufu na kwa sababu mapungufu haya yapo katika kila upande, mara utasikia wodi ya wazazi, mara wodini. Sasa kuna kikwazo gani kwa Wizara ya afya kuweka vitambulisho vya wafanyakazi wakavaa beji ili wale wafanyakazi wazuri wakajulikana na wale ambao wanazembea kazi wakajulikana kirahisi na kuripotiwa badala ya kuwa kila mmoja daktari ni kikwazo gani kilichopo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, mapungufu yote aliyoyasema Mhe. Mjumbe sasa hivi yote yameshafanyiwa kazi, isipokuwa suala (b) kuhusu wafanyakazi wazuri hili nataka kusema wafanyakazi wetu wote wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ni wazuri.

Kuhusu suala la vitambulisho hilo tunalifanyia kazi na limeshaanza hivi sasa kwa upande wa wauguzi, ile kuweka kila mmoja na nafasi yake kujulikana huyu ni muuguzi, huyu Mfamasia, huyu mtu wa lebo na huyu ni *orderly* hizo taratibu tunaziandaa. Lakini wafanyakazi wote ni wazuri sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, mimi kwa upande wangu niseme tu kwamba wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii nawapongeza kwa dhati kwa juhudi zao mbali mbali hasa yanapotokea maafa katika sehemu mbali mbali hushiriki kikamilifu ili kunusuru jamii ambayo inahitaji mahitaji yale, lakini katika suala (b) limeeleza kwamba kuna wafanyakazi wangine au baadhi ya wafanyakazi sio wote wazuri na sio wote wabaya, lakini tuamini kwamba binaadamu wote sio sawa.

Je, kwa kuwa kilio hichi kipo cha muda mrefu na huwa sugu wakati mwengine kwa sababu unapomwendea pale panapotolewa dawa mtu kashughulika na mazungumzo yake hata hana habari na wewe akakupa dawa uende zako. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ina mpango gani wa kutoa taaluma zaidi kunusuru jamii yetu isiathirike na madawa haya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Kwanza nizipokee pongezi zake kwa Wizara yetu pamoja na wafanyakazi wote kwa niaba yao nimezipongea na nitawafikishia wenyewe tukijaaliwa.

La pili anasema kwenye mazuri basi na mabaya kidogo yanakuwepo, nasema kama lipo tatizo hilo tulisema tokea mwanzo kwamba yoyote atakayebainika katika sehemu yake hawajibiki vizuri basi tuletewe taarifa mara moja na hatua tutazichukua, kama nilivyosema kwamba hakuna mchele usiokuwa na chuwa basi hizo chuwa huwa tunazifanyia kazi.

Nam. 2

Wataalamu Kutowatembelea Wakulima

Mhe. Ashura Abeid Faraji – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatumia pesa nyingi katika kuwapatia wafanyakazi wake taaluma ya kilimo ili baadaye elimu hiyo isambazwe kwa Wakulima. Chakusikitisha Wataalamu hao wanapomaliza mafunzo hayo hubakia afisini na wala hawaitoi taaluma hiyo kwa Wakulima kama ilivyotarajiwa.

(a) Mhe. Waziri, katika hali hiyo huoni kuwa Serikali inashindwa kufikia lengo lake la kuimarisha kilimo nchini.

(b) Ni sababu zipi zinazowafanya Wataalamu hao kushindwa kuwatembelea Wakulima wetu na kujua matatizo yanayowakabili.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 2 lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Wataalamu wa Kilimo baada ya kumaliza mafunzo yao hupangiwa kazi kutokana na mahitaji halisi ya Wizara, aidha mahitaji makubwa ya Wataalam hao yapo vijijini na Wilayani. Hali halisi inaonyesha kwamba kuna upungufu wa mabwana shamba. Hivi sasa bwana shamba mmoja anahudumia wakulima wapatao 1,500 wakati kiutendaji na kwa ufanisi zaidi bwana shamba mmoja anatakiwa kuwafikia wakulima 400 tu.

Kwa asilimia kubwa wataalam hao hupangiwa kazi katika wilaya hizo za Zanzibar ukiacha Wilaya ya Mjini Unguja, ndani ya Wilaya hizo wanapangiwa kuzi kuanzia ngazi ya Shehia kama mabwana shamba, wataalam wa fani maalum *subject meter specialist* pia wapo wataalam kwenye ngazi ya wilaya hadi Mikoa. Wote hawa husaidiana na mabwana shamba kwa kutoa elimu kwa wakulima, kwa mfano tumeanzisha skuli za wakulima mabwana shamba darasa 360 ambao wanasaidiwa na *program* ya AST, taaluma nyengine zinatolewa kupitia mradi wa *PADEP* ambapo hapo awali mradi huu ulikuwa ukisimamiwa wilaya tano tu, lakini sasa tumeongeza wilaya nne zaidi hivyo kufanya wilaya zote kutekelezwa na mradi huu.

(b) Mhe. Spika, Wataalamu wetu wanafika kwa wakulima lakini mara nyingi huwafikia wakulima ambao wapo katika vikundi, na linapotokezea tatizo lolote mabwana shamba wetu katika ngazi ya Shehia huliripoti kwa Wataalam wa Juu na hatua za haraka huchukuliwa. Aidha, kitengo cha habari na vielelezo kiliopo chini ya Kamisheni ya Kilimo, Utafiti na Elimu kwa Wakulima, hutoa taaluma/taarifa mbali mbali juu ya kilimo bora na chenye tija kwa wakulima, kama matumizi ya mbegu bora, mbolea na kadhalika.

Mhe. Spika, hivi sasa Wizara yangu kupitia Waziri mwenyewe wa Kilimo, Mifugo na Mazingira imeshatoa taarifa kipindi kirefu sana

kwa wataalam wetu kujipangia *program* maalum ambayo tutaonyesha kila mwezi wamefanya kazi vipi katika vijiji vyetu na kuwafikia shamba pamoja na matatizo makubwa kwamba wao ni kidogo na wanaohitaji taaluma za kilimo ni wengi.

Lakini pia naomba Mhe. Spika, kupitia Baraza lako hili tukufu kama wanavyofanya wafugaji wetu, tunawaomba na wakulima pale linapojitokeza tatizo basi wasione tabu kufuata wataala wetu na milango ya Wizara yetu iko wazi kwa Unguja na Pemba, pia watufikie ili tuweze kuendeleza kilimo hiki na zaidi katika kipindi hiki kigumu ambacho nchi imekabiliwa na njaa, hivyo tunahitaji kulima kiziada na kiutaalam.

Mhe. Ashura Abeid Faraji: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri haoni kwamba hivi sasa kuna mazao yanapungua sana kutokana na wataalam kuwasomesha sana lakini hawapitii wakulima, zamani walikuwa wakipitia wataalam pamoja na Wakuu wa Mikoa siku hizi mambo yote Afisi tu na wakati tunakabiliwa na hali ya uchumi ngumu, hebu tutokeni tufunge vibwebwe na tufunge mikanda.

Mhe. Spika, tupitie katika mashamba kujua mazao gani yatapatikana kwa wingi na mazao gani yana matatizo, mihogo mpaka sasa hivi ni migonjwa, binaadamu nae ana ungojwa wa mambo kama hayo.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri jibu swali hilo kwa nini mazao yamepungua kwa sababu ya mabwana shamba na maombi kupitia hayo kwa sababu pia ameomba.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo, Mazingira: Kwanza ushauri wake tunauchukua kama nilivyosema mwanzo kwamba wataalam wetu wawe wanafuata na kufanya kila jitihada lakini ni kidogo sana kuwahudumia, lakini nataka nimhakikishie kwamba tutazidisha jitihada za mwisho kabisa kuhakikisha kwamba sasa hawa wataalam wasiwe wanakaa pale afisini na wawe wanakwenda kutoa taaluma kwa wakulima wetu kwa ziada.

Lakini suala la kwamba kuna maradhi kama alivyosema kuna maradhi kwa binaadamu pia kwa mihogo zaidi, nataka tukubaliane kwamba ni kweli yapo maradhi ya mihogo na wataalam wetu huwa wanatoa taaluma kwa kutumika zile mbegu ambazo tumezifanyia utafiti kwa sasa hivi ambazo zitakuwa zinastahamili maradhi zaidi, kwa hivyo na wakulima wetu wazikubali zile mbegu mpya ambazo zimeanzishwa na wataalam wetu.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu a, b, na c.

Kwanza napenda kumuuliza Mhe. Waziri kwa kuwa kumsomesha mkulima hasa ambae bahati mbaya hakupata elimu ya kutosha ya darasani kunahitaji zaidi kuona kuliko kusikia.

a) Je, haoni kwamba ipo haya hawa mabwana na mabibi shamba wanaotoa elimu kwa wakulima kwamba na wao wawe na mashamba ya mfano kama wanavyofanya wenziwao Tanzania Bara.

b) Kwa kuwa hawa Mabwana shamba na mabini shamba wanahitaji utaalam wa uhakika wanapowasaidia wakulima, haoni kwamba ipo haja kwa sasa hawa mabwana shamba na mabibi shamba wawe na elimi inayoanzia *diploma* na sio *certificate* tena.

c) Je, haoni haja ya kufanya utafiti ili kubaini kwa nini hawa mabwana shamba na mabini shamba hawapiti kama alivyozungumza Mhe. Ashura Abeid Faraji kwa sababu wakati wa ukoloni kuliwa na hawa mabwana samba wakati huo waiitwa marenja walikuwa wanapita na walikuwa wakali sana, Je, haoni kwamba ipo haja ya kufanya utafiti Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kuona kwamba kwa nini wakati wa ukoloni hawa walikuwa wanafanya kazi, lakini baada ya Mapinduzi wataalam wetu wanashindwa kufanya kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Kwanza naomba nikubaliane na suala lake

(a) kama alivyotueleza kwamba kuwasomesha au kuwapa taluma watu ambao hawakupata elimu ya madarasa ni vigumu, sasa inatakiwa kuwapa taaluma kwa njia ya kuona. Kwa hivyo nakubaliana nae tutafanya jitihada zetu kuhakikisha wataalam wetu na wao wanalima katika meeneo yale, japo maeneo mengi ambayo nimetembelea kule Pemba nimebaini baadhi ya wataalam wetu na wao wanalima katika maeneo yale, sasa kule kwenye mapungu ambako wataalam hawalimi basi hilo ni agizo ambalo tutalifanyia kazi.

(b) Kwamba wataalam wetu sasa hivi tunaowasomesha wasiishie ngazi ya cheti, hili tunalichukua na Wizara tutalifanyia kazi kuhakikisha kwamba Chuo chetu kinatoa

ngazi ya Diploma, kwa sababu ni kweli kwa sasa hivi tunatoa katika ngazi ya *Certificate*.

(c) Utafiti a kuwajua watu wetu lengo hili ambalo Mhe. Waziri amelianzisha la kwamba wawe wana *programe* maalum inaonyesha wanafanya kazi zao vipi kwa mwezi, lengo kubwa wametutaka na wao leo watusikie. Napenda kumhakikishia kwamba moja katika lengo letu kubwa sasa hivi ni kutaka kujua zile kazi zao wanazifanya vipi ndio maana tukawataka wawe na *programe* maalum, kwa hivyo Wizara sasa itawafuatilia kwa ziara zaidi kuweza kujua ni kweli wamefanya hilo jambo na tukaangalia zile *program* zao walizofanya.

Naa tukibaini kwamba kuna watu wanatudanganya hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa muda mrefu wataalam wengi tulipata kusikia kwamba wamehama nchi kutokana na kuwa maslahi yao madogo hawatengenezewi maslahi ya kuridhisha, naomba kuuliza hili lina ukweli gani.

Lakini pili kwa kipindi kirefu mbawana shamba na mabibi shamba wanalalamika sana kwamba wana nia nzuri ya kufanya kazi lakini kinachowapa tabu ni vipando, je, Wizara yeke ina utaratibu gani wa kuwapatia vipando ili wakulima wafikiwe na mabwana shamba na mabibi shamba.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kwanza amesema anataka kujua hawa wataalam wanaohama kutokana na maslahi, kiukweli hatuwezi kujua kiuhakika kwa sababu mtu akiamua kuacha kazi na kwenda kutafuta maslahi mengine kile mmoja na wazo lake, lakini kiufupi ni kwamba watu wanaacha kazi na sio wizara yetu tu au hapa Zanzibar tu lakini ni utaratibu maalum au mtindo kwa baadhi ya wananchi kuamua na zaidi kutafuta maslahi.

Lakini kuhusu *scheme of service* ni moja katika tatizo kwa sababu wapo wafanyakazi wengi bado wapo nchini na wanaendelea nayo. Lakini napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba *scheme of service* Wizara yangu imo katika kuitengeneza na kuiwasilisha serikalini haraka iwezekanavyo kwa wafanyakazi wote.

Jambo jengine ni kwamba mabwana shamba hawa moja katika matatizo ambayo hawafiki katika maeneo yao kwa kuwafuatilia wakulina na kuwasaidia kwa kuwapa elimu, pengine ni kutokana na shida au upungufu wa vipando. Ni kweli hapo nyuma tulikuwa na tatizo hilo, lakini napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba chini ya mradi huu wa Kilimo na Mifugo miradi hii miwili ni mikubwa sana, wizara imeshaanza kuchukua hatua za kuwapatia vipando mabwana na mabibi shamba na itaendelea kufanya hivyo kuhakikisha kwamba kila bwanashamba ana kipando.

Mhe. Spika, kwa kuwa muda wa maswali umemalizika na kazi inayofuata sasa hivi ni kusoma bajeti, lakini kwa utaratibu wetu huwa tunasoma bajeti saa 10.00 jioni lakini taratibu zinatuelekeza tuitishe kikao saa 11.00 jioni. Hivyo nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi atuombe sisi Wajumbe na tukubali kuitisha kikao chetu saa 10.00 jioni kwa ajili ya kusoma bajeti, na wakati huo huo tukubali kwamba tuvunje muda huu hadi wakati huo tukajitayarishe kwa hapo jioni.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Masuala ya Fedha (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, naomba kuotoa hoja ya kuliahirisha Baraza lako kabla ya wakati wake na pia hii leo tuje saa 10.00 jioni badala ya saa 11.00 kama kawaida yetu kwa wakati wa jioni kwa madhumuni ya kuja kusikiliza hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 4.00 Asubuhi kikao kiliahirishwa mpaka Saa. 10.00 jioni)

(Saa 10:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Hotuba ya Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa ruhusa

yako naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa likae kama Kamati Maalum, ili liweze kupokea, kujadili na hatimae kuidhinisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010.

Pamoja na hotuba hii naomba pia kuwasilisha vitabu vinavyoelezea kwa kina Mpango wa Serikali na Bajeti kwa mwaka huo. Kitabu cha kwanza kinahusu Mapitio ya Hali ya Uchumi na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo katika mwaka 2008/09, kitabu cha pili kinahusu Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2009/2010 na kitabu cha tatu ni Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia afya na uzima na kuweza kukutana tena hii leo katika kikao hiki cha kuyajadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2009/2010. Tunamuomba Mwenyezi Mungu akijaalie kikao hiki kiweze kuendesha kazi zake kwa amani, usalama utulivu na upendo kati yetu ili tuweze kuyafikia malengo yaliyokusudiwa *(Makofi)*.

Kwa mara nyengine tena sina budi kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Amani Abeid Karume kwa uongozi wake wa hekima na busara katika kuiongoza nchi yetu *(Makofi)*.

Naomba kumshukuru sana Mhe. Rais kwa maelekezo na muongozo ambao amekuwa akitupatia ndani ya Wizara ya Fedha na Uchumi katika kazi zetu za kila siku. Upeo na uzoefu mkubwa wa mambo ya fedha na uchumi alionao Mhe. Rais umekuwa ukitusaidia sana katika mwenendo mzima wa kuiongoza wizara hii ambayo ndio roho ya serikali nzima.

Mhe. Spika, naomba kuitumia fursa hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wizara ya Fedha na Uchumi, kukushukuru wewe binafsi kwa kuliongoza vyema Baraza hili. Pia Wizara ya Fedha na Uchumi inamshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, pamoja na Wajumbe wake.

Aidha, shukurani pia ziwaendee Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa mchango wao mkubwa katika maandalizi ya bajeti hii ninayoiwasilisha hivi sasa. Ushauri, mapendekezo na maelekezo waliyoyatoa katika kila wizara, yamesaidia sana kuifanya bajeti hii iwe bora zaidi. Mchango wao umetuwezesha kufanya marekebisho muhimu na kurahisisha utayarishaji wa bajeti za wizara mbali mbali.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009 unaotarajiwa kumalizika hivi karibuni, Baraza letu limepata misiba miwili kwa kuondokewa na wenzetu Mhe. Daud Hassan Daud wa Jimbo la Magogoni na Mhe. Soud Yussuf Mgeni wa Jimbo la Wawi. Mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya Wizara ya Fedha na Uchumi, naomba kutoa mkono wa pole kwako na kwa familia za marehemu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema wenzetu hao waliotangulia mbele ya haki.

Naomba pia kuitumia fursa hii kutoa pole kwa wenzetu wote waliopatwa na msiba kutokana na tukio la kuzama kwa meli ya MV. Fatih lilitokea katika Bandari ya Malindi hapa Unguja tarehe 29 Mei mwaka huu. Tunawaomba wafiwa wote wawe na subira pamoja na wale waliopoteza mali zao kutokana na kadhia hii kubwa na wakati huu serikali imeunda Tume maalum kuchunguza chanzo cha ajali hiyo.

Mhe. Spika, naomba pia nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Asha Moh'd Hilal kwa kuchaguliwa kwa wingi wa kura kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Magogoni kwa tiketi ya CCM. Matumaini yetu kuwa ataitumia vyema imani aliyopewa na Chama cha Mapinduzi kuwa Mgombea wake na wananchi wa Magogoni kuwa Mwakilishi wao kwa kuendeleza juhudi za kuwaletea maendeleo katika jimbo hilo *(Makofi)*.

Tokea mwanzoni mwa miaka ya 2000, serikali imekuwa ikitekeleza Mpango wake wa muda mrefu wa Maendeleo ujulikanao kama Dira ya 2020 (Vision 2020). Inatarajiwa kuwa utekelezaji wa Dira hii kuu ya Maendeleo utasaidia kujenga uchumi imara unaohimili ushindani katika medani ya kimataifa, kuondoa kabisa umasikini uliokithiri nchini na kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi.

Mhe. Spika, ili kutekeleza Dira ya 2020 kwa kipindi cha 2007 hadi 2010, serikali ilizindua Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA) mwanzoni mwa mwaka 2007. Ripoti ya utekelezaji wa MKUZA 2007/2008 iliyotolewa mwezi wa Novemba 2008, inaelezea kwa kina maendeleo yaliyofikiwa, changamoto zilizopo na hatua zaidi za kuchukuliwa, ili kufikia malengo yaliyowekwa kwa ufanisi zaidi.

Mafanikio hayo ni pamoja na kukua kwa uchumi kwa wastani wa asilimia 6.2 baina ya 2006 na 2007. Aidha, deni la Taifa lilipungua kwa asilimia 33 katika kipindi hicho, sambamba na ukuaji wa mapato uliofikia asilimia 18.2 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2007/08 kutoka 16.3 kwa mwaka 2006/07. Kwa upande wa elimu, kumekuwa na mafanikio katika uandikishaji wa wanafunzi kwa skuli za chekechea uliongezeka kufikia asilimia 22.2 kwa mwaka 2007 kutoka asilimia 15.9 mwaka 2005.

Aidha, kwa upande wa elimu ya msingi uandikishaji ulifikia asilimia 104 mwaka 2007 kutoka 93.8 kwa mwaka 2006 na kiwango cha wanafunzi waliofaulu kidato cha pili katika elimu ya sekondari imefikia asilimia 50.9 mwaka 2007 kutoka asilimia 46.9 mwaka 2005.

Vile vile jitihada za serikali za kutafuta rasilimali zaidi za kutekeleza MKUZA zilizaa matunda, kwa kuwezesha kutekelezwa miradi mikubwa ya miundombinu kama vile ya kupelekwa umeme Pemba kutoka Tanga, miradi mbalimbali ya Barabara, ukamilishaji wa ujenzi wa Gati ya Malindi, na mradi wa kuweka njia mpya ya umeme baina ya Ras Kiromoni na Fumba. Maelezo kamili yanapatikana katika Ripoti ya Utekelezaji wa MKUZA (*Makofi).*

Mhe. Spika, kipindi cha utekelezaji wa MKUZA kilikabiliwa na changamoto kadhaa zilizopelekea kutofikiwa kwa malengo yote ya MKUZA. Miongoni mwa changamoto hizo ni kupanda kwa bei za vyakula na mafuta duniani zilizopelekea kuongezeka kwa mfumko wa bei na msukosuko wa Soko la Fedha Duniani, ambayo kwa ujumla wake yalipelekea kudorora kwa uchumi na hivyo kupunguza mafanikio yaliopatikana katika juhudi za kupunguza umasikini.

Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA) na ule wa Tanzania Bara (MKUKUTA) inamalizika muda wake kwa pamoja mwishoni mwa mwaka wa fedha 2009/2010. Mikakati bora zaidi inahitajika ili kuendeleza utekelezaji wa malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa (Dira ya 2020) kuanzia mwaka wa fedha 2010/2011.
Mhe. Spika, ili kuandaa mikakati hiyo, mapitio ya utekelezaji wa MKUZA yanafanywa sambamba na MKUKUTA, ikiwa ni jitihada za kuoanisha mipango ya kitaifa pamoja na upatikanaji wa fedha. Mchakato wa mapitio haya unatarajia kuonesha hali ya sasa ya umasikini na kubainisha maeneo mapya ya kuwekewa nguvu zaidi.

Mapitio ya Hali ya Uchumi na Msukosuko wa Uchumi Duniani

Mhe. Spika, wakati nawasilisha hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2008/2009, nilizungumzia changamoto mbali mbali kutoka nje zinazoukabili uchumi wetu. Kwa bahati mbaya nyingi ya changamoto hizo zimeendelea kuwepo na kuongezeka zaidi katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti.
Miongoni mwa hizo, changamoto kubwa zaidi na yenye athari ya moja kwa moja kwa uchumi wa Zanzibar ni msukosuko wa soko la fedha duniani. Athari za msukosuko huu zinajitokeza kwenye utulivu wa uchumi, kupungua kwa mahitaji na bei za bidhaa na huduma zinazozalishwa na nchi zinazoendelea kama Zanzibar, na kupunguka kwa uwekezaji na misaada kutoka nje. Aidha,

msukosuko huu unatarajiwa pia kupunguza misaada inayotumwa na jamaa kutoka nje.

Mhe. Spika, kulingana na makadirio ya mtazamo wa uchumi wa dunia katika miaka ya usoni uliotolewa na Shirika la Fedha la dunia (IMF) Aprili 2009, uchumi wa dunia unakisiwa kushuka kwa asilimia 1.3 mwaka 2009 kutoka ongezeko la asilimia 3.2 mwaka 2008. Nchi zilizoendelea uchumi wake utashuka kwa asilimia 3.8 mwaka 2009 kutoka ongezeko la asilimia 0.8 mwaka 2008. Kwa nchi zinazoendelea, matarajio ni kushuka hadi kufikia asilimia 1.6 mwaka 2009 kutoka asilimia 6.1 mwaka 2008.

Kwa upande wa Afrika, inakadiriwa ukuaji wa uchumi kushuka hadi asilimia 2.0 mwaka 2009 kutoka asilimia 5.2 mwaka 2008. Kasi ya ukuaji wa uchumi katika nchi zilizo Kusini ya Jangwa la Sahara itapungua kutoka asilimia 5.4 mwaka 2008 hadi kufikia asilimia 2.9 mwaka 2009. Kushuka huku kunasababishwa na kupungua kwa utashi wa bidhaa na huduma pamoja na kupungua kwa rasilimali za uwasilishaji na hivyo kupungua kwa uzalishaji.

Mhe. Spika, kwa upande wa mfumko wa bei, msukosuko wa fedha utapelekea kushuka kwa mfumko hadi kufikia asilimia 0.3 mwaka 2009 kutoka asilimia 3.4 mwaka 2008 kwa nchi zilizoendelea.

MAPITIO YA HALI YA UCHUMI NA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA ZANZIBAR 2008/09

Mapitio ya Hali ya Uchumi 2008/09 Sekta ya huduma yaendelea kuongoza katika ukuaji wa uchumi na wastani wa pato la mtu wazidi kuimarika

a) **Pato la Taifa**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa 2008 ukuaji wa uchumi ulitarajiwa ufikie asilimia 6.8. Ukuaji halisi umefikia asilimia 5.4. Kasi hii ya ongezeko imepungua kwa asilimia 14 ikilinganishwa na ukuaji wa uchumi wa asilimia 6.3 kwa mwaka 2007. Sekta ya huduma imeendelea kuongoza katika ukuaji wa uchumi. Sekta hii imekua kwa kasi ndogo ya asilimia 6.4 ikilinganishwa na asilimia 10.4 kwa mwaka 2007.

Ukuaji wa sekta hiyo kwa mwaka 2008 ulichangiwa zaidi na sekta ya usafirishaji na mawasiliano ambayo imekua kwa asilimia 28.9. Kwa upande mwengine, kupungua kwa kasi ya ukuaji wa Sekta hiyo ya Huduma ni matokeo ya kushuka kwa asilimia kumi kwa idadi ya watalii walioingia nchini kutoka 143,265 mwaka 2007 hadi 128,440 kwa mwaka 2008.

Kasi ya ukuaji kwa sekta ya kilimo imeongezeka kwa asilimia 5.7 mwaka 2008 kutoka ukuaji pungufu wa asilimia 0.4 mwaka 2007. Ukuaji huo kwa mwaka 2008 umechangiwa zaidi na ukuaji wa uzalishaji wa mazao ya kilimo ulioongezeka kwa asilimia 6.5 na hasa mazao ya biashara pamoja na kuimarika kwa Sekta ya Uvuvi, hasa uvuvi wa samaki kwa asilimia 5.2.

Mhe. Spika, ukuaji wa uchumi wa asilimia 5.4 kwa mwaka 2008, umepelekea Pato la Taifa lifikie TSh. 747,950 milioni ikilinganishwa na TSh. 586,388 milioni mwaka 2007 kwa bei za mwaka husika. Pato la mtu binafsi liliongezeka kwa wastani wa asilimia 23.8 kutoka TSh. 516,000 ambazo ni sawa na dola za Kimarekani 414 mwaka 2007 na kufikia TSh. 639,000 sawa na dola za Kimarekani 534 mwaka 2008.

Vichocheo vikuu vya ukuaji huo wa uchumi ni pamoja na hali nzuri ya hewa hasa mvua, iliyoimarisha shughuli za kilimo pamoja na utoaji wa mbegu bora na usambazaji wa mbolea kwa wakulima. Vichocheo vyengine ni pamoja na ushindani katika utoaji wa huduma za mawasiliano ya simu, kuongezeka kwa idadi ya abiria wanaosafiri kwa njia ya bahari kutoka 1.3 milioni hadi 1.4 milioni pamoja na kuongezeka kwa mwenendo wa ukuzaji rasilimali kutoka TSh. 129,429 milioni mwaka 2007 hadi TSh. 145,151 milioni mwaka 2008. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 22 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2007 na asilimia 19 kwa mwaka 2008.

Mchango wa Sekta katika Pato la Taifa

Mhe. Spika, Sekta ya Huduma ndio yenye mchango mkubwa katika Pato la Taifa kwa kuchangia wastani wa asilimia 42.6 ya pato lote. Kiwango hicho kimepungua kwa asilimia 3.4 ikilinganishwa na mchango wa wastani wa asilimia 44.1 kwa mwaka 2007.

Kushuka kwa mchango wa Sekta ya Huduma kunatokana na kukua kwa kasi zaidi kwa sekta ya kilimo na kupungua kwa mchango wa sekta ndogo ndogo zote katika sekta ya jumla ya huduma isipokuwa kwa sekta ya usafiri na mawasiliano.

Kwa upande wa Sekta ya Kilimo kwa mwaka 2008, imechangia wastani wa asilimia 30.8 ya pato lote la Taifa. Kiwango hicho kimeongezeka kwa asilimia 12.0 ikilinganishwa na mchango wa wastani wa asilimia 27.5 kwa mwaka 2007 kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kwa asilimia 25.7.

Mfumko wa Bei

Mhe. Spika, Mfumko wa Bei umeendelea kuwa ni changamoto kubwa kwa mwaka 2008. Mfumko huo ulifikia wastani wa asilimia 20.6 kwa mwaka 2008 kutoka wastani wa asilimia 13.1 kwa mwaka 2007. Sababu za kiwango hiki cha juu cha mfumko huo ni pamoja na mambo yafuatayo:-

1. Kuendelea kupanda kwa bei za mafuta katika kipindi chote cha miezi tisa ya mwanzo ya mwaka 2008, kulikopelekea gharama za uzalishaji na huduma kama usafiri kuwa za juu.

2. Mfumko wa Bei kwa bidhaa za chakula umeonekana kuwa na kiwango kikubwa zaidi na kufikia wastani wa asilimia 24.3 kwa mwaka 2008, wakati kwa bidhaa zisizo za chakula, ikiwemo mafuta, ulifikia wastani wa asilimia 16.6. Hata hivyo katika miezi ya hivi karibuni, mwenendo wa mfumko wa bei umeonesha kushuka na kufikia asilimia 12 kwa mwezi wa Aprili na asilimia 9 kwa mwezi wa Mei 2009.

   Ongezeko la bei za mafuta ya petroli na chakula ndizo zinazochangia zaidi mfumko wa bei hapa nchini. Kwa Zanzibar chakula kinachukua uzito wa asilimia 57.4 ya mkoba wa bidhaa zinazozingatiwa katika kupima mfumko wa bei. Uzito huo kwa Zanzibar unatokana na mchele wenye uzito wa wastani wa asilimia 21 na samaki wenye uzito wa zaidi ya asilimia 13 na kufanya jumla ya uzito wa bidhaa hizi muhimu kuwa zaidi ya asilimia 34.

Hali ya Deni la Taifa

Mhe. Spika, jumla ya Deni la Taifa hadi kufikia Machi 2009 ni TSh. 137,809.75 milioni, sawa na asilimia 23.4 ya Pato la Taifa. Kati ya deni hilo, deni la nje ni TSh. 81,200 milioni na deni la ndani lilifikia TSh. 56,609.75 milioni. Deni la ndani linajumuisha hati fungate, dhamana za serikali, malipo ya wastaafu, wazabuni na mashirika ya serikali.

Kati ya deni la nje la TSh. 81,200 milioni sawa na dola za Kimarekani 61.5 milioni; TSh. 60,700 milioni sawa na dola za Kimarekani 46.0 milioni limedhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na bakaa ya TSh. 20,500 milioni sawa na dola za Kimarekani 15.5 milioni ni madeni yasio na udhamini. Serikali itahakikisha madeni yanalipwa wakati muafaka kwa utaratibu uliopo.

Mhe. Spika, napenda kutoa taarifa kwa Baraza lako Tukufu kwamba kwa sasa malipo ya mafao ya wastaafu yanaendelea kulipwa mara tu taratibu za uhakiki wa malipo zinapokamilika. Deni la wastaafu lililosalia hadi mwezi Machi, 2009 ni la kipindi cha miezi miwili tu (Februari na Machi, 2009) *(Makofi)*.

HALI YA BIASHARA

Biashara na Nchi za Nje

Mhe. Spika, mwenendo wa sekta ya biashara na nchi za nje umeonesha hali nzuri katika kipindi cha mwaka 2008. Usafirishaji wa bidhaa kwenda nje umekuwa kwa asilimia 42.6 baina ya 2007 na 2008 kutoka thamani ya TSh. 21,177.7 milioni mwaka 2007 hadi TSh. 30,189.2 milioni mwaka 2008. Uingizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi umeshuka kutoka TSh. 107,689.9 milioni mwaka 2007 hadi TSh. 93,439.6 milioni mwaka 2008 sawa na upungufu wa asilimia 13.2.

Mwenendo huo wa usafirishaji na uingizaji umepelekea kupungua kwa nakisi katika urari wa biashara kwa asilimia 7.7 kutoka nakisi ya TSh. 68,512.8 milioni mwaka 2007 hadi TSh. 63,250.4 milioni mwaka 2008.

Kwa upande wa mazao, zao la karafuu bado limekuwa ni tegemeo la nchi kwa kuingiza fedha za kigeni ingawa Sekta ya Huduma (utalii) ndio inayoongoza kwa sasa. Katika kipindi cha mwaka 2008 thamani ya karafuu zilizouzwa nchi za nje imeongezeka na kufikia TShs. 15,878 milioni ikilinganishwa na mwaka 2007 ambapo mauzo yalikuwa TSh. 10,527 milioni.

Zao jengine lililojipatia umaarufu na kuwa tegemeo la wananchi wengi hasa akina mama wa vijijini, Unguja na Pemba, ni zao la mwani. Jumla ya tani 11,293 zilisafirishwa nje kwa mwaka 2007, ambazo ziliweza kuingiza nchini jumla ya TSh. 2,989 milioni. Thamani ya mwani uliyosafirishwa nchi za nje imeongezeka kwa asilimia 16.8 na kufikia TShs. 3,492 milioni mwaka 2008

Mhe. Spika, mwenendo mzuri wa hali ya biashara umejitokeza pia kwa upande wa biashara na Tanzania Bara. Usafirishaji wa bidhaa zilizozalishwa nchini uliongezeka kutoka thamani ya TSh. 968.2 milioni mwaka 2007 hadi TSh. 1,479.6 milioni mwaka 2008 sawa na ongezeko la asilimia 52.8.

Bidhaa zinazoingia nchini kutoka Tanzania Bara zilipungua kwa asilimia 6, kutoka TSh. 27,608.5 milioni hadi TSh. 25,936.5 milioni mwaka 2008. Hali hii imepelekea kushuka kwa nakisi ya urari wa biashara na Tanzania Bara kwa asilimia 7.9 kutoka nakisi ya TShs. 26,640.3 milioni mwaka 2007 hadi TShs. 24,456.9 milioni mwaka 2008.

HUDUMA YA SEKTA YA FEDHA

Mhe. Spika, maendeleo ya kiuchumi ya nchi yoyote hutegemea sana upeo na ufanisi wa sekta yake ya fedha. Kwa muda mrefu sekta hii muhimu ilikuwa finyu na hivyo kutoa mchango mdogo katika maendeleo ya nchi. Kwa msaada wa Benki ya Dunia, Tanzania imekua katika harakati za mageuzi ya sekta hii muhimu chini ya awamu ya pili ya programu ya mageuzi ya sekta ya fedha (*Second Generation Financial Sector Reform*).

Lengo kuu la programu hii ambayo inatekelezwa kwenye maeneo ya Benki za Biashara, benki ndogo ndogo, taasisi za bima, mifuko ya hifadhi ya jamii, mifuko ya kuchangia na kukopa na kadhalika na kuifanya sekta hii nchini kuwa mchangiaji halisi wa uchumi wa Tanzania.

Kwa upande wa Zanzibar sekta hii kwa sasa, inajumuisha Benki za Biashara, Asasi ndogo ndogo za fedha (*Micro-finance Institutions*), mashirika na makampuni ya Bima, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, na maduka ya kubadilishia fedha (*Bureau de change*). Kwa ujumla, sekta hii bado ni changa na ina fursa ya kuimarika zaidi na kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mhe. Spika, uwekaji wa amana katika Benki za Biashara umeongezeka hadi kufikia TSh. 209,100 milioni mwezi Machi 2009 ikilinganishwa na TSh. 161,200 milioni zilizowekwa kama amana mpaka kufikia Machi 2008 sawa na ongezeko la asilimia 29.7. Uwiano wa amana kwa Pato la Taifa nao umefikia wastani wa asilimia 28.0 Machi 2009, ikilinganishwa na asilimia 27.5 mwezi Machi 2008.

Kwa upande wa ukopeshaji, mikopo iliyotolewa na Benki ziliopo Zanzibar imeongezeka kwa asilimia 49.6 na kufikia TSh. 62,400 milioni mwishoni mwa mwezi wa Machi 2009 kutoka TSh. 41,700 milioni mwezi Machi 2008. Uwiano wa mikopo na amana nao umeongezeka kutoka asilimia 25.9 Machi 2008 hadi kufikia asilimia 29.9 mwezi Machi 2009. Ongezeko hili linaashiria muamko wa kutumia huduma za mikopo kwa sekta ya watu binafsi ikijumuisha waajiriwa katika taasisi mbali mbali za serikali na kampuni hapa Zanzibar.

Changamoto Zinazokabili Maendeleo ya Uchumi wa Zanzibar

Mhe. Spika, mbali ya mafanikio tuliyoyaonesha kuhusiana na uchumi wetu, bado kuna changamoto za ndani na nje zinazoathiri ukuaji endelevu wa uchumi wetu. Miongoni mwa changamoto za ndani ni pamoja na kasi kubwa ya ukuaji wa idadi ya watu, uzalishaji mdogo wa mazao ya chakula, mifugo na samaki, udogo wa Sekta ya Viwanda, uchanga wa Sekta ya Fedha pamoja na kiwango cha chini cha usafirishaji bidhaa nje ya nchi.

Mhe. Spika, kiwango cha ukuaji wa idadi ya watu kiliopo cha asilimia 3.1 ni kikubwa sana na kinapelekea kuongezeka kwa kasi kubwa zaidi ya mahitaji ya jamii kama vile elimu, afya na makaazi kwa kulinganisha na ukuaji wa uchumi wetu.

UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI 2008/09

Mapitio ya Mapato na Matumizi ya Serikali 2008/09
Mapato ya Serikali yanaendelea kuimarika zaidi

Mhe. Spika, kwa mwaka 2008/09, serikali ilijipangia kukusanya jumla ya mapato ya ndani ya TSh. 134,550 milioni ikiwa ni asilimia 17 zaidi ya makadirio ya mwaka 2007/08 ya TSh. 114,560 milioni. Utekelezaji halisi hadi mwezi Machi 2009 ulifikia asilimia 76.7 ya makadirio ya mwaka, sawa na TSh. 103,232.5 milioni. Matarajio ya makusanyo hadi Juni 2009 ni kufikia TSh. 134,500 milioni sawa na asilimia 99.9 ya lengo. Matarajio haya yanaonesha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani unaotokana na juhudi kubwa za usimamizi wa mapato ya serikali kupitia taasisi za ukusanyaji mapato za *ZRB* na *TRA*.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2008/09 Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) ilitarajiwa kukusanya jumla ya TSh. 49,371 milioni sawa na asilimia 36.7 ya mapato ya ndani. Hadi Machi 2009 tayari *TRA* ilikusanya TSh. 39,415.78 milioni sawa na asilimia 79.8 ya lengo la mwaka. Kati ya makusanyo hayo, ushuru wa forodha umefikia TSh. 24,781.4 milioni sawa na asilimia 82.8 ya lengo la mwaka.

Mhe. Spika, makusanyo ya ushuru wa uagiziaji yamefikia TShs. 10,275.5 milioni sawa na asilimia 89.3 ya makadirio ya mwaka. Kwa ujumla, mapato yatokanayo na forodha yameongezeka kwa asilimia 39 ikilinganishwa na kipindi cha miezi tisa kwa mwaka 2007/08. Hali hii imechangiwa zaidi na usimamizi mzuri wa mapato hayo pamoja na kuimarika kwa huduma za bandari baada ya matengenezo ambayo yalikamilika rasmi mwezi Disemba 2008. Kwa upande wa makusanyo yatokanayo na kodi ya mapato yalifikia TSh.

14,634.4 milioni sawa na asilimia 75.9 ya makadirio ya mwaka, ambapo Mamlaka ilipanga kukusanya jumla ya TSh. 19,274.8 milioni. Matarajio halisi ya makusanyo kwa Mamlaka ya Mapato hadi Juni 2009 ni kufikia TSh. 51,608.8 milioni sawa na asilimia 104.5 ya lengo la mwaka 2008/09.

Mhe. Spika, Bodi ya Mapato ya Zanzibar (*ZRB*) kwa mwaka 2008/09 ilipanga kukusanya TSh. 73,543 milioni sawa na asilimia 54.7 ya mapato yote ya ndani kabla ya kuzingatia mapato ya Mawizara. Hadi kufikia mwezi Machi 2009, *ZRB* tayari ilikusanya TSh. 56,996.1 milioni sawa na asilimia asilimia 77.5 ya makisio ya mwaka.

Mhe. Spika, mapato yatokanayo na kodi ya ongezeko la thamani (*VAT*) yamefikia jumla ya TSh. 28,086.6 milioni sawa na asilimia 73.8 ya makadirio ya mwaka. Vyanzo vya mapato ambavyo kwa sehemu kubwa vinachangiwa na mwenendo wa sekta ya utalii (kodi zinazotokana na hoteli na mikahawa) vimefikia jumla ya TSh. 1,539.3 milioni sawa na asilimia 97.7 kwa mwaka kwa upande wa mahoteli na jumla ya TSh. 762.9 milioni sawa na asilimia 74.7 kwa upande wa mikahawa. Hadi mwezi Juni 2008 Bodi inatarajiwa kukusanya jumla ya TSh. 72,456 milioni sawa na asilimia 98.5 ya makadirio ya mwaka.

Mhe. Spika, mapato yasiyokuwa ya kodi kwa mwaka 2008/09 yalikadiriwa kufikia TSh. 9,841 milioni. Makusanyo halisi kwa kipindi cha Julai-Machi 2008/09 yamefikia TSh. 6,820.6 milioni sawa na asilimia 69.3 ya makadirio ya mwaka. Matarajio halisi kwa vianzio visivyokuwa vya kodi hadi Juni 2009 ni kufikia TSh. 9,785.1 milioni sawa na asilimia 99.4 ya lengo la mwaka.

Makisio na Matumizi ya Serikali kwa Kazi za Kawaida

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi ya kawaida ya serikali, jumla ya TSh. 102,614 milioni zilitumika hadi kufikia Machi 2009 ikiwa ni sawa asilimia 69 ya makadirio ya mwaka ya TSh. 149,435 milioni. Kati ya matumizi hayo, jumla ya TSh. 47,900 milioni zilitumika kwa kulipia mishahara ya mawizara ambayo ni sawa na asilimia 75 ya makadirio ya mwaka ya TSh. 64,094 milioni. Matumizi mengineyo yamefikia jumla ya TSh. 21,603 milioni ambazo ni sawa na asilimia 67 ya makadirio ya mwaka ya TSh. 32,358 milioni.

Mhe. Spika, matumizi ya Mfuko Mkuu wa Hazina yalifikia jumla ya TSh. 21,946 milioni sawa na asilimia 63 ya makadirio ya mwaka ya TSh. 35,107 milioni. Aidha, matumizi yanayohusiana na ruzuku kwa taasisi za serikali yalifikia jumla ya TSh. 11,165 milioni kwa kipindi cha miezi tisa sawa na asilimia 63 ya makadirio ya mwaka ya jumla ya TSh. 17,821 milioni.

Misaada kutoka nje

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2008/09 serikali ilitarajia kupokea mapato yanayotokana na misaada ya kibajeti (4.5%) yenye jumla ya TSh. 23,407 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Hadi kufikia Machi 2009, jumla ya TSh. 22,907 milioni tayari zimepatikana sawa na asilimia 98 ya lengo la mwaka. Utekelezaji huo unatokana na utaratibu wa kutanguliza malipo hayo kwa serikali kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kama ilivyokubaliwa chini ya Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA).

Makisio na Matumizi Halisi ya Misaada kwa Programu na Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2008/09

Mhe. Spika, jumla ya TSh. 173,752 milioni zilikisiwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2008/09. Hadi kufikia mwezi Machi 2009 jumla ya TSh. 43,410.2 milioni sawa na asilimia 24.9 zilitumika kwa madhumuni hayo. Aidha serikali ilipokea TSh. 6,878.8 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ambazo zimetumika moja kwa moja katika miradi iliyopo katika sekta. Kwa ujumla fedha zote zilizopokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kutokana na misaada na mikopo pamoja na misaada ya kibajeti ni TSh. 73,196 milioni.

UTEKELEZAJI WA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO
Kuongeza Ada ya Uwanja wa Ndege

Mhe. Spika, Serikali ilirekebisha kiwango cha Ada ya Uwanja wa Ndege kwa abiria wanaokwenda nje ya nchi kutoka dola za Kimarekani 25 hadi 30 kuanzia Julai 2008. Katika utekelezaji wa hatua hiyo kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2008 hadi Machi 2009, jumla ya TSh. 5,016.2 milioni zimekusanywa ikilinganishwa na ukusanyaji wa TSh. 4,491.0 milioni uliofanywa katika kipindi kama hicho kwenye mwaka wa fedha uliopita 2007/2008. Hivyo kumejitokeza ongezeko la mapato ya TSh. 525.2 milioni ambayo ni sawa na asilimia 11.69

Kuimarisha ukusanyaji wa vianzio visivyokuwa vya Kodi
Mhe. Spika, serikali kupitia Bodi ya Mapato Zanzibar imefanya tathmini ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya vianzio vyote vya mapato ya Mawizara na Taasisi zake na kutoa mapendekezo mbali mbali ya kuimarisha taratibu za ukusanyaji na usimamizi wa mapato hayo ya Mawizara .

Katika kipindi hiki cha miezi tisa, jumla ya TSh. 6,820.6 milioni zilikusanywa ikilinganishwa na ukusanyaji wa TSh. 5,827.40 milioni uliofanywa katika kipindi cha miezi kumi na mbili ya mwaka wa fedha uliopita 2007/2008.

Ushuru wa kukuza ujuzi

Mhe. Spika, serikali ilifanya marekebisho katika Sheria ya Kuanzisha Vyuo vya Amali nchini. Marekebisho hayo yalihusu kuanzisha tozo inakayojulikana kama Ushuru wa Kukuza Ujuzi ambayo imepitishwa na kuanza kukusanywa rasmi kuanzia Julai 2008. Katika utekelezaji wa hatua hiyo kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2008 hadi Machi 2009, jumla ya TSh. 2,135.5 milioni zilikusanywa.

Kupitia na Kuweka Viwango Vipya vya Kodi ya Ardhi

Mhe. Spika, **s**erikali katika jitihada zake za kuimarisha mapato ilikusudia kupitia na kuweka viwango vipya vya kodi ya ardhi, kupitia taratibu zake na kuandaa mikakati ya ugombozi wa madeni. Katika utekelezaji wa hatua hiyo kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2008 hadi Machi 2009, jumla ya TSh. 1,055.6 milioni zilikusanywa.

Ushuru wa Bidhaa kwenye Bia, Sigara na Ulevi Mkali

Mhe. Spika, Serikali imepitia viwango vya ushuru wa biashara na kutoza TSh. 400/= kwa lita ya bia na ulevi mkali na TSh. 500/= kwa kila sigara 1000. Katika kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2008 hadi Machi 2009, jumla ya TSh. 1,416.1 milioni zimekusanywa ikilinganishwa na ukusanyaji wa TSh. 919.7 milioni uliofanywa katika kipindi kama hicho kwenye mwaka wa fedha uliopita 2007/2008 kabla ya utozaji huo kuanza. Hivyo kumejitokeza ongezeko la mapato ya TSh. 496.4 milioni ambazo ni sawa na asilimia 53.97

Kuanzishwa kwa Kodi ya Majengo

Mhe. Spika, Serikali imekusudia ifikapo Julai 2009 kuanzisha Kodi ya Majengo nchini kwa lengo la kuimarisha mapato ya ndani. Mapato haya yamekusudiwa kuongeza uwezo wa Serikali za Mitaa, Mabaraza ya Miji na Baraza la Manispaa la Zanzibar katika kuhudumia shughuli za utawala na kuchangia miradi ya maendeleo inayohusu huduma za kichumi na kijamii.

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa hatua hiyo, Serikali imeshapitisha Sheria mpya ya Kodi ya Majengo ambapo utekelezaji wake utaanza rasmi mwaka ujao wa fedha.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI 2008/09

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2008/2009 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipanga kutekeleza programu 20 na miradi 63 ya maendeleo. Kati ya programu na miradi hiyo, programu 13 na miradi 21 ya maendeleo ilitekelezwa katika Klasta ya Ukuzaji Uchumi na Upunguzaji Umasikini wa Kipato, programu mbili na miradi 26 ilitekelezwa katika Klasta ya Huduma za Kijamii na Ustawi na programu tano na miradi 16 ilitekelezwa katika Klasta Utawala Bora na Umoja wa Kitaifa. Aidha, ndani ya programu hizo ilikuwemo miradi ya sekta mtambuka ambayo ilijumuishwa ndani ya Klasta zote tatu.

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2008/2009 jumla ya TSh. 192,273.8 milioni zilipangwa kutumika ikijumuisha mchango wa Serikali, misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo TSh. 18,522.0 milioni sawa na asilimia 9.6 ya bajeti yote ya maendeleo ni mchango wa Serikali, TSh. 173,752 milioni sawa na asilimia 90.4 ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zikiwemo TSh. 101,324.8 milioni ruzuku na TSh. 72,427.0 milioni mikopo.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2008 hadi Machi 2009, jumla ya TSh. 61,527.5 milioni sawa na asilimia 32 ya bajeti ya maendeleo zilitolewa. Kati ya fedha hizo, Serikali ilitoa TSh. 18,117.37 milioni sawa na asilimia 29.45 na Washirika wa Maendeleo wamechangia TSh. 43,410.15 milioni sawa na asilimia 70.55 ya matumizi ya maendeleo. Mchango wa Serikali kwa kipindi hicho umefikia asilimia 98 na mchango wa Washirika wa Maendeleo umefikia asilimia 35.33 ya makadirio ya mwaka.

Mhe. Spika, fedha zilizotolewa na Serikali katika utekelezaji wa programu/miradi ya maendeleo zimeongezeka kutoka TSh. 10,163.6 milioni mwaka 2007/2008 hadi kufikia TSh. 18,117.4 milioni mwaka 2008/2009 sawa na ongezeko la asilimia 36.4. Kumekuwa na ongezeko la programu na miradi iliyotekelezwa kutoka programu 16 na miradi 60 mwaka 2007/2008 hadi kufikia programu 20 na miradi 63 mwaka 2008/2009. Aidha, upatikanaji wa fedha kwa utekelezaji wa programu na miradi umefikia asilimia 98. Sababu kuu ni kuongezeka kwa ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya Serikali ambayo yametokana na usimamizi mzuri wa vyanzo vya mapato pamoja na elimu kwa walipa kodi.

Mhe. Spika, maelezo ya kina ya utekelezaji halisi wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2008/09 yanapatikana katika kitabu cha Kwanza cha

Mapitio ya Hali ya Uchumi na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2008/09 ambacho kimesambazwa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu sambamba na hotuba hii.

MIRADI MIDOGO MIDOGO YA WANANCHI

Mhe. Spika, kama ilivyo ada, Serikali imeendelea kusaidia nguvu za wananchi kwa miradi inayoibuliwa na wananchi wenyewe katika maeneo yao. Miongoni mwa miradi iliyopatiwa fedha ni ya barabara (miradi kumi na moja), vituo vya maji (miradi kumi na mbili), ujenzi wa skuli (miradi ishirini na moja), ujenzi wa soko (miradi miwili), kilimo (miradi miwili) na vituo vya afya (miradi miwili). Kati ya miradi hiyo, miradi 29 yenye thamani ya TSh. 107 milioni imetekelezwa Unguja na miradi 33 yenye thamani ya TSh. 88.5 milioni imetekelezwa Pemba na kufanya jumla ya fedha zote zilizotolewa kwa kusaidia nguvu za wananchi katika miradi yao midogo midogo kufikia TSh. 195.5 milioni sawa na asilimia 54.3 ya makadirio ya mwaka kwa TShs. 360 milioni. *(Makofi).*

UTEKELEZAJI WA MAENEO YALIYOPEWA MSISITIZO ZAIDI WA KITAIFA MWAKA 2008/09

Mhe. Spika, ili kuweza kufikia malengo ya ukuaji wa uchumi endelevu na kupunguza umasikini kwa wananchi walio wengi hasa vijijini, mpango wa maendeleo wa mwaka 2008/09 uliweka msisitizo zaidi kitaifa katika maeneo yafuatayo:

i) Miradi ya kilimo
ii) Huduma za jamii – hasa Afya
iii) Upatikanaji wa maji safi na salama
iv) Kuimarisha elimu
v) Kuimarisha miundombinu ya mawasiliano na nishati.
vi) Vita dhidi ya ukimwi na madawa ya kulevya
vii) Kuyashirikisha makundi mbali mbali ya kijamii katika maendeleo ya nchi

Kuongeza uwekezaji kwenye miradi ya sekta ya kilimo kwa lengo la kutoa mazao yenye kuhitajika katika soko la utalii vile vile mazao ya kukidhi mahitaji ya soko la ndani na la nje ili kuimarisha biashara.

Mhe. Spika, katika kufikia azma hii, hatua mbali mbali zimechukuliwa ambazo zinasaidia katika kuweka mazingira bora ya mahusiano baina ya sekta ya kilimo na utalii na biashara. Serikali imewapatia mafunzo wakulima 5,780 juu ya mbinu bora za uzalishaji wa mazao na uhifadhi wa mazingira kutokana na uanzishwaji wa mashamba-darasa 217 kupitia miradi ya ASSP na ASDP/L.

Mhe. Spika, aidha tafiti mbali mbali zimefanywa ikiwemo wadudu waharibifu wa mazao ya mboga mboga na muhogo kwa kutumia madawa ya asili na mbolea. Matokeo ya awali ya utafiti huo yanaonesha kupungua kwa maradhi kati ya asilimia 40 hadi 55.

Mhe. Spika, chini ya Programu ya Usimamizi wa Maliasili, mafunzo ya uhifadhi wa misitu, ufugaji nyuki na kazi za mikono yametolewa kwa wanajamii. Pia mafunzo ya kilimo mchanganyiko cha mikarafuu yametolewa kwa wakulima 78 Unguja na Pemba. Mafunzo ya uchumaji na ukaushaji wa zao la karafuu yametolewa kwa wakulima 55. Jitihada za kuendeleza zao la karafuu zinaendelea kuchukuliwa ambapo jumla ya miche 300,000 ya mikarafuu imeoteshwa kwa Unguja na Pemba. Vile vile, jumla ya miti 7,000 ya mazao ya biashara imezalishwa ikiwemo Mikungu Manga, Mihiliki, Midalasini, Mitangawizi, Manjano, Pilipili Manga, Mibuni na Mivanila pamoja na miche 400,000 ya minazi.

Mhe. Spika, kazi za ujenzi wa miundo mbinu ya umwagiliaji maji katika maeneo ya Uzini, Mgenihaji, Matetema na Kitogani ziko katika hatua nzuri ambapo zaidi ya asilimia 60 ya kazi imetekelezwa. Aidha kazi za Uvunaji maji zimefanyika katika maeneo ya Kibokwa, Koani na Kiboje kwa Unguja na Pemba katika maeneo ya Weni na Kwapweza. Uwekezaji huu wa sekta ya kilimo utaimarisha uzalishaji wa mazao ya chakula na ya biashara ambao utaleta faida kwa wakulima na kuimarisha mahusiano na sekta ya utalii na biashara.

Mhe. Spika, mwaka jana nililieleza Baraza lako tukufu kuwa Serikali imeunda Kamati ya Kuimarisha kilimo. Ninafuraha kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa Kamati hiyo imekamilisha kutayarisha Mkakati wa Kuimarisha Kilimo na tayari umeshapitishwa na Serikali. Mkakati huo utasaidia sana kuimarisha kilimo cha mazao ya chakula pamoja na azma ya kuongeza uzalishaji ili kuwa na chakula cha kutosha na kupunguza uagiziaji.

Kutoa kipaumbele kwa sekta za huduma za jamii hususan huduma za chanjo, mama wajawazito ili kupunguza vifo vya mama na watoto, kuimarisha usambazaji maji safi mijini hususan katika miji ya Chakechake, Wete na Mkoani.

Mhe. Spika, kampeni ya chanjo ya watoto wenye umri wa miezi 6 hadi miaka 10 ilifanyika kwa asilimia 88 pamoja na kupatiwa jenereta jipya la kisasa ili lisaidie kuhifadhia dawa za chanjo. Kampeni ya chanjo ya kimataifa ya surua, matone ya vitamini A na dawa za minyoo imefanyika pamoja na ufuatiliaji wa kazi za chanjo katika ngazi za wilaya. Vile vile, chanjo mpya ya kukinga

watoto dhidi ya maradhi ya homa ya uti wa mgongo na homa ya mapafu imetolewa katika vituo vyote vya afya vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, katika juhudi za kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto, wodi ya wazazi katika hospitali ya Mnazi Mmoja ilipatiwa vifaa mbali mbali na utaratibu wa utekelezaji *(Road map)* kuzinduliwa wenye ujumbe wa **"uzazi bila ya vifo inawezekana kama kila mmoja atatekeleza wajibu wake"**. Aidha, mafunzo ya miongozo ya kitaifa ya utoaji wa huduma za afya yametolewa kwa wakuu wa vituo vya afya vya Unguja na Pemba. Pia jumla ya vituo 26 vya Unguja na Pemba vinatoa huduma ya kuzuia maambukizi ya Virusi Vinavyosababisha Ukimwi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Mhe. Spika, kwa upande wa sekta ya Maji katika miji ya Chakechake, Wete na Mkoani, Serikali tayari imetiliana saini ufadhili wa mradi huo na Benki ya Maendeleo ya Afrika na uzinduzi rasmi wa utekelezaji wa mradi ulifanyika tarehe 4 Mei, 2009. Aidha, mradi wa kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama kwa mji wa Chake Chake unaofadhiliwa na taasisi isiyo ya Kiserikali ya *"Ivo de Carneri"* umeanza na kufanya tathmini ya ubora wa maji na unaendelea kwa kuchimba visima, kuweka pampu na kubadilisha mabomba ya zamani ya *'Asbestos Cement'* na kuweka mapya.

Mhe. Spika, katika kuongeza huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama mijini, matayarisho ya awamu ya pili ya ujenzi wa mradi mkubwa wa maji katika Mkoa wa Mjini/Magharibi yameanza na utiaji saini kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Japan. Hafla hiyo ilifanyika tarehe 26 Februari 2009. Aidha Serikali tayari imetiliana saini na Mkandarasi wa utekelezaji wa mradi huo. Mradi huu unajumuisha ujenzi wa matangi mawili eneo la Dole na Kinuni, uchimbaji wa visima vitano huko Kinumoshi na Kimara na ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilomita 19.9

Upatikanaji wa maji safi na salama vijijini Unguja na Pemba kwa lengo la kupunguza maradhi ya miripuko.

Mhe. Spika, kazi ya usambazaji maji vijijini imekamilika kwa vijiji vya Jambiani Mfumbwi, Buyu, Mji Mpya, Kijichame Ole-Kianga, Shumba Mjini, Uroa-Pongwe, Ole-Kipangani, Dunga na Kiguuni ambapo wananchi wanafaidika na huduma ya maji. Kazi za ulazaji wa mabomba, uchimbaji wa visima na ujenzi wa matangi kwa miradi ya maji katika vijiji vya Tumbatu, Miwani, Kigongoni, Chaani Kubwa, Kizimkazi Dimbani na Mkunguni, Koani, Kidimni, Gombani-Kwale na Ubago zinaendelea. Aidha, matayarisho kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji safi na salama na usafi wa mazingira kwa vijiji tisa vya Nungwi, Matemwe, Dunga/Tunguu na Machui kwa Unguja na vijiji

vya Kambini, Vitongoji, Mizingani, Wambaa na Ndagoni kwa Pemba, yamefanyika.

Kuimarisha elimu katika ngazi zote pamoja na kuendelea kukuza vipaji vya watendakazi kwa kutoa mafunzo.

Mhe. Spika, Serikali imeandaa Mpango wa Elimu wa Muda Mrefu wa Zanzibar wa mwaka 2008/09 - 2015/16 na Mpango wa Muda Mfupi ambao utekelezaji wake unaanza mwaka 2009/10 hadi mwaka wa fedha wa 2011/12. Utekelezaji wa mipango hiyo ni sehemu ya mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Elimu ya mwaka 2006. Katika hatua za uimarishaji wa sekta ya Elimu, jumla ya vitabu 930,000 vya ngazi ya sekondari (165,000 Baiolojia, 165,000 Kemia na 600,000 Hisabati) vimechapishwa na kusambazwa katika skuli za Unguja na Pemba. Pia, Serikali inakusudia kuimarisha elimu ya sekondari kwa kukamilisha uchapishaji na ununuzi wa vitabu vya kufundishia sekondari kwa masomo yaliyobakia ya sayansi jamii, biashara na kompyuta, sanaa, lugha ambapo kila mwanafunzi atakuwa na vitabu vya kutosha vya masomo yote ya elimu ya sekondari.

Aidha, jumla ya wanafunzi 437 wamepatiwa mikopo ya masomo katika vyuo mbali mbali, kati ya hao wanafunzi 400 wanasoma vyuo vya ndani na 37 vyuo vya nje. Jumla ya wanafunzi 358 walijiunga na vyuo vikuu, kati ya hao wanafunzi 336 wanasoma vyuo vya ndani na 22 vyuo vya nje. Wakati huo huo, mafunzo maalum kwa walimu wa maandalizi yametolewa juu ya matumizi ya muhtasari mpya wa elimu ya maandalizi na mafunzo ya ualimu kwa walimu wa kawaida yametolewa katika vituo vya ualimu Unguja na Pemba.

Kuimarisha miundombinu ya bandari, barabara, nishati na viwanja vya ndege pamoja na huduma za usalama Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, matengenezo ya bandari ya Malindi yamekamilika na uzinduzi ulifanyika tarehe 9 Januari 2009. Kufuatia kukamilika kwa ujenzi huo shughuli za bandari pia zimeimarika. Katika kipindi cha Januari-Aprili 2009, idadi ya makontena yaliyoingizwa nchini imefikia 4,464 ikilinganishwa na makontena 3,006 yaliyoingizwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2008 ikiwa ni ongezeko la makontena 1,458. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya meli kubwa za mizigo 10 zenye uzito wa tani 91,945 zimeingia bandarini ikilinganishwa na meli ndogo ndogo 11 zenye uzito wa tani 61,752 zilizoingia bandarini katika kipindi hicho mwaka 2008. Kwa upande mwengine, mapato ya ushuru wa Forodha nayo yameongezeka ambapo katika kipindi cha Januari-Mei 2009, mapato yamefikia TSh. 15,008 milioni ikilinganishwa na TSh. 11,289 milioni zilizokusanywa kwa kipindi kama hicho mwaka 2008. Ongezeko hilo ni kiasi cha TSh. 3,819 milioni.

Mhe. |Waziri Wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa upande wa barabara, ujenzi wa barabara za Kinyasini-Tunguu (km 26.8), Pongwe-Matemwe (km 20.4) na Mkoani-Makombeni (km 6.5) tayari umekamilika. Aidha, ujenzi wa Barabara ya Mazizini-Fumba (km 18.4) na Mshelishelini-Pwanimchangani (km 6.5) unaendelea vizuri. Aidha, mkataba wa ujenzi wa barabara za Wete-Konde (km 15.1), Wete-Gando (km 13) na Wete-ChakeChake (km 29) umeshasainiwa na mkandarasi yuko katika matayarisho ya kuanza kazi. Kuhusu barabara sita za Kusini Pemba za Chanjamjawiri-Tundaua (km 10), Chanjaani-Pujini (km 5), Mtambile-Kengeja-Mwambe (km 9.4), Kenya-Chambani (km 3.2), Mizingani-Wambaa (km 9.7), na Mtambile-Kangani (km 6.4), nina furaha kulijuilisha Baraza lako tukufu kuwa ujenzi wa barabara hizo ambao ulisita mwaka jana na fedha zake kuhaulishwa kupelekwa katika mradi wa umeme wa Tanga-Pemba, hivi sasa unaendelea tena.
Mhe. Spika, jitihada za kupatikana kwa huduma ya umeme wa uhakika katika kisiwa cha Pemba zinaendelea vyema ambapo utiaji saini mkataba wa utengenezaji wa waya wa baharini baina ya Serikali na kampuni ya NEXANS ya Norway umefanyika tarehe 22 Agosti 2008. Kutokana na mpango wa kazi za mradi huu, kazi ya utandazaji wa waya wa umeme kutoka Tanga hadi Pemba inatarajiwa kukamilika mwezi Disemba mwaka huu wa 2009.

Mhe. Spika, matayarisho kwa ajili ya utandazaji wa waya mpya wa umeme kutoka Ras Kiromoni hadi Fumba chini ya msaada wa Serikali ya Marekani katika mpango wa MCC yanaendelea vizuri. Tathmini ya nyumba na mazao ya wananchi watakaoathirika na mradi huu tayari imeshafanywa. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tayari imetenga fedha kwa ajili ya ulipaji wa fidia. Aidha hatua za kutafuta mkandarasi wa kutekeleza mradi huu zinaendelea. Matarajio ni kwamba mradi huu utakamilika mwishoni mwa mwaka 2012. Jitihada za kupata majenereta ya dharura kwa Unguja nazo pia zinaendelea.

Mhe. Spika, kwa upande wa uimarishaji wa viwanja vya ndege, matengenezo ya dharura ya njia ya kurukia na kutua ndege katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Zanzíbar yamefanyika kuwezesha ndege kutua na kuruka kama kawaida. Mkandarasi wa matengenezo ya kuongeza urefu wa njia ya kurukia na kutua kutoka mita 2,462 za sasa hadi kufikia mita 3,022 pamoja na matengenezo ya sehemu ya kuegeshea ameshapatikana.

Maeneo mengine yaliopewa mkazo ni kuongeza juhudi za mapambano dhidi ya kuenea virusi vya ukimwi na madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, katika juhudi za kupunguza maambukizo mapya ya virusi vya ukimwi, jumla ya vituo 26 vinatoa huduma ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Jumla ya vituo 41 vimetoa huduma za ushauri nasaha na upimaji damu wa hiari kwa Unguja na Pemba. Aidha, tathmini imefanywa ya utumiaji wa dawa ya ARV katika hospitali ya Mwembeladu, Al Rahma na Micheweni ambapo huduma hizo tayari zimeshaanza kutolewa na kwa kuanzia huduma zinatolewa wiki mara moja.

Mhe. Spika**,** katika kupambana na madawa ya kulevya na kurekebisha tabia, jumla ya skuli 36 zilitembelewa zenye wastani wa wanafunzi 4,160 wakiwemo wanaume 1980 na wanawake 2180 na kupatiwa taaluma ya athari za matumizi ya madawa ya kulevya.

Kuendeleza utamaduni wa kuyashirikisha makundi mbali mbali ya jamii katika mchakato wa maendeleo ya nchi.

Mhe. Spika, ushiriki wa wadau katika kupanga, kutekeleza na kufuatilia mipango ya maendeleo ni jambo la msingi na Serikali imekusudia kuliendeleza. Katika mwaka 2008/09 wadau wameshirikishwa ipasavyo katika mchakato wa maendeleo ya nchi. Katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa MKUZA wadau wote wakiwemo Jumuia zisizokuwa za Kiserikali wanashiriki katika kamati zote za ufuatiliaji. Aidha Jumuia hizi hufanya tathmini ya matumizi ya fedha za umma na kutoa ushauri kwa Serikali.

Mhe. Spika, kwa kutambua umuhimu wa makundi mbali mbali ya jamii, Serikali imesaidia kujenga uwezo wao kwa kuandaa mafunzo na kuwapatia misaada ya kitaaluma na kifedha kila inapobidi. Lengo ni kuimarisha uwezo wao ili ushiriki wao katika mchakato wa maendeleo uwe wa manufaa zaidi kwao na kwa jamii yote. Katika kipindi hiki Serikali imefanya vikao viwili vya Baraza la Biashara (ZBC) ambapo wadau wote walishiriki kikamilifu. Kutokana na mwenendo mzuri wa majadiliano kati ya Serikali na sekta binafsi, Serikali imeweza kuyatambua matatizo ya wafanyabiashara na kuanza kuyachukulia hatua zifaazo. Pia wafanyabiashara wamekubali wito wa Serikali wa kuonesha nia ya kuafiki ulipaji wa kodi stahiki kwa hiari na kwa wakati.

MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA 2009/10

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza hapo mwanzoni, kutokana na sababu za msukosuko wa uchumi unaoendelea duniani hivi sasa ambao unatarajiwa kuwa na athari kwa uchumi wa nchi zinazoendelea ikiwemo Zanzibar. Matarajio kwa

mwaka 2009 ni kushuka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi hadi kufikia asilimia 4.9 kutoka kasi ya asilimia 5.4 ya mwaka 2008. Kama nilivyoeleza, shughuli zinazotarajiwa kuathirika zaidi ni zile zinazotegemea mauzo katika masoko ya nje kama vile utalii na shughuli zinazogharamiwa kwa fedha kutoka nje ikiwa ni pamoja na uwekezaji wa mitaji na rasilimali.

Mhe. Spika, ili kukabiliana na athari za msukosuko huo kwa nchi yetu, Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania iliunda kikosi kazi chini ya uenyekiti wa Gavana wa Benki kuu, ili kuangalia njia na namna ya kukabiliana na athari kwa uchumi wa Tanzania kutokana na msukosuko wa fedha pamoja na kuporomoka kwa uchumi duniani. Zanzibar iliwakilishwa na wataalamu watatu katika kikosi kazi hicho. Serikali ilifanya uamuzi huo kutokana na ukweli kwamba Tanzania imeungana na mfumo wa fedha wa dunia kwa kupitia biashara ya bidhaa na huduma kati yake na nchi nyengine duniani, mitaji ya kimataifa inayoingia na kutoka Tanzania, na bei za bidhaa na huduma katika soko la kimataifa. Kikosi hicho kimeandaa na kuwasilisha katika serikali zetu mbili mpango wa kujinusuru na athari za msukosuko huo *(Rescue Plan).*
Mhe. Spika, sekta ambazo zimeanza kuonesha athari kwa upande wa Zanzibar ni utalii ambako kumeonekana kushuka kwa idadi ya wageni wanaoingia nchini ambapo mapato ya utalii yanatarajiwa kushuka kwa asilimia 10. Sekta nyengine ni kilimo ambapo pameonekana kushuka kwa bei ya zao la karafuu na mwani katika soko la dunia.

Mhe. Spika, hatua za mkakati wa kujinusuru umezingatia mambo yafuatayo:

(i) Kupunguza makali au kuhimili shindikizo la msukosuko hususan kuwalinda wananchi walio katika hatari kubwa zaidi;
(ii) Kuhakikisha uendelevu wa ukuaji uchumi kwa kupunguza gharama za uwekezaji na uzalishaji.

Mhe. Spika, mkakati huu wa kunusuru uchumi unazingatia mihimili muhimu ifuatayo:

(i) Kulinda ajira na vipato kwa mwaka 2009 na 2010.
(ii) Kuhakikisha upatikanaji wa chakula *(Food security)*
(iii) Kulinda program muhimu za kijamii, pamoja na
(iv) Kulinda uwekezaji muhimu kwa maendeleo ya nchi.

Mhe. Spika, mbali ya mkakati huo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wa utalii, imechukua hatua za haraka kukabiliana na tatizo hilo kwa kuangalia upya masoko yetu na kuupitia mfumo mzima wa utalii wetu ili kuendelea kuwashawishi wageni kuja Zanzibar. Jitihada zinafanywa kuimarisha utalii wa kikanda kwa kuwashajiisha wenye mahoteli kuweka viwango maalum vya malipo na kuandaa kampeni kubwa ya kujitangaza. Kwa sasa nguvu zaidi zimeelekezwa katika masoko yanayoibuka *(emerging*

markets) kama Urusi, Nchi za Scandinavia, Mashariki ya Mbali, Nchi za Kiarabu na Afrika ya Kusini. Hatua za kufuatilia masoko hayo zimeanza kuchukuliwa na matarajio yanategemewa kuwa mazuri.

Mhe. Spika, Kwa kuzingatia athari za msukosuko wa fedha na kupunguza makali ya athari kwa wananchi, pamoja na kuhakikisha soko la utalii, Serikali imeamua kupunguza kodi ya ongezeko la thamani kutoka asilimia 20 ya sasa hadi asilimia 18. Mkakati huu unategemea kupunguza mapato ya Serikali kwa kadiri ya TSh. 2,000 milioni ambapo Serikali inatarajia kuziba pengo hilo kutokana na kuongezeka kwa ushajiishaji wa ulipaji wa kodi kwa hiari *(tax compliance).*

Mfumko wa bei

Mhe. Spika**,** mfumko wa bei kwa mwaka 2008 ulifikia asilimia 20.6 kutoka asilimia 13.1 mwaka 2007 kufuatia ongezeko la bei ya mafuta na chakula mwaka 2007/08. Mfumko wa bei kwa mwaka 2009 unatarajiwa kupungua hadi asilimia 13.0, hali inayotokana na kushuka kwa bei ya mafuta na bidhaa nyengine kutoka nje pamoja na kuyumba kwa uchumi wa dunia. Aidha, kupungua kwa bei za chakula pamoja na hatua za makusudi zinazochukuliwa za kupambana na ongezeko la ujazi wa fedha ni vichocheo vya kupungua kwa mfumko wa bei unaotarajiwa. Pamoja na matarajio hayo mfumko wa bei unaweza kuathirika iwapo bei za mafuta zitaongezeka sambamba na kuongezeka kwa bei za bidhaa kutoka nje.

MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWAKA 2009/2010

Mhe. Spika, Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2009/2010 utaendelea kuzingatia Dira ya Maendeleo ya 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA) na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Kutokana na umuhimu mkubwa uliopo wa kuleta maendeleo mijini na vijijini, Serikali imetenga jumla ya TSh. 40,725.1 milioni kugharamia jumla ya programu 22 na miradi 65 ya maendeleo kwa mwaka wa 2009/2010. Kima hichi cha rasilimali kwa mwaka 2009/2010 ni kikubwa kwa ongezeko la TSh. 22,203.1 milioni sawa na asilimia 119.9 ikilinganishwa na kile kilichotengwa kwa mwaka 2008/2009. Ongezeko kubwa lililochangia katika kukuza kiwango cha bajeti ni nia ya Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kuhakikisha kwamba miundombinu ya upatikanaji wa umeme wa uhakika; usambazaji wa maji safi na salama na matengenezo na ujenzi wa barabara

ndani ya visiwa hivi inakamilika ili kuongeza chachu ya maendeleo nchini. *(Makofi).*

Mhe. Spika, miongoni mwa programu na miradi iliyopangwa, zipo progaramu 3 na miradi 12 mipya. Katika mchakato huu wa bajeti ya kugharamia miradi na programu za maendeleo, Serikali inatarajia kupata kutoka kwa Washirika wa Maendeleo jumla ya TSh. 199,187.78 milioni ikiwa ni mikopo na misaada ya kimaendeleo. Kwa ujumla bajeti ya kazi za maendeleo inakadiriwa kuwa TSh. 239,912.88 milioni. Hii ni sawa na asilimia 58.1 ya bajeti yote ya Serikali.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Klasta ya kukuza uchumi na Kupunguza Umasikini wa Kipato inatarajiwa kutekeleza jumla ya programu 14 na miradi 21 ya maendeleo itakayogharimu jumla ya TSh. 145,724.28 milioni sawa na asilimia 60.74 ya bajeti ya maendeleo. Klasta ya Huduma na Ustawi wa Jamii imepanga kutekeleza programu 3 na miradi 28. Kati ya hiyo miradi 5 mipya. Jumla ya TSh. 80,418.66 milioni sawa na asilimia 33.52 ya bajeti yote ya maendeleo. Klasta ya Utawala Bora na Umoja wa Kitaifa imepanga kutekeleza programu 5 na miradi 16 ambapo miradi 4 ni mipya. Jumla ya TSh. 13,769.95 milioni sawa na asilimia 5.74 ya bajeti yote ya maendeleo.

MWELEKEO WA BAJETI 2009/2010

Mhe. Spika, katika hatua ya maandalizi na utayarishaji wa bajeti ya mwaka ujao wa fedha 2009/2010, Serikali imezingatia ushirikishwaji wa wadau mbali mbali ikiwemo sekta ya watu binafsi. Serikali imeunda Kikosi Kazi cha Mikakati ya Ukusanyaji wa Mapato na Mageuzi ya Mifumo ya Kodi *(Tax Reform Task Force)* iliojumuisha wajumbe kutoka katika taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali pamoja na asasi mbali mbali nchini.

Mhe. Spika, naomba kulijuilisha Baraza lako Tukufu kwamba miongoni mwa hatua za kuimarisha mapato zitakazochukuliwa katika mwaka ujao wa fedha 2009/2010 na kupendekezwa katika bajeti ni baadhi tu ya maoni na ushauri uliotolewa na kamati hiyo. Hatua hii ni muhimu katika kuimarisha ushirikishwaji wa wananchi katika maandalizi ya bajeti ya Serikali na vile vile kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika suala zima la usimamizi wa ukusanyaji wa mapato nchini.

Mhe. Spika, nina furaha kulitangazia Baraza lako tukufu kwamba kauli mbiu ya Bajeti ya mwaka 2009/2010 ni **Bajeti ya Maendeleo ya Miundombinu kwa kuimarisha Kilimo na Utalii**. Mhe. Spika, hii ni bajeti ya Miundombinu kwa maana kwamba asilimia 33 ya bajeti imekwenda katika kugharamia shughuli za nishati, maji, barabara na viwanja vya ndege. Kwa mwaka ujao wa fedha, matumizi ya maendeleo yanaendelea kuwa makubwa ikilinganishwa na

matumizi ya kazi za kawaida ambapo yamefikia asilimia 58.1 ya bajeti yote. Hii inadhihirisha wazi dhamira ya serikali katika kujenga misingi imara ya ukuaji wa uchumi na kuleta maendeleo endelevu kwa jamii.

Mapato ya ndani
Mhe. Spika, kutokana na mwelekeo wa makusanyo halisi kwa mwaka 2008/09 kufikia asilimia 99.9, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 2009/10 inatarajia kukusanya jumla ya TSh. 159,697 milioni kutokana na vyanzo vyake vya mapato ya ndani. Kati ya mapato hayo, TSh. 148,932 milioni yatatokana na kodi na TSh. 10,765 milioni yatatokana na vyanzo visivyokuwa vya kodi.

Kati ya mapato yatokanayo na kodi TSh. 85,773 milioni yatakusanywa na ZRB na TSh. 63,159 milioni zitakusanywa na TRA.

Mapato ya Nje
Mapato ya misaada ya kibajeti 2009/10

Mhe. Spika, matarajio ya misaada ya kibajeti ya asilimia 4.5 kwa mwaka 2009/10 yamefikia TSh. 50,214.1 milioni. Kati ya mapato hayo TSh. 34,175 milioni yatatokana na ruzuku na TSh. 16,039.1 milioni yatatokana na mikopo.

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa kwa mara ya kwanza katika mwaka ujao wa fedha 2009/2010, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itafaidika kupata asilimia 4.5 ya misaada ya kibajeti kutokana na mikopo *(GBS Loan)* tokea Tanzania ilipoanza kufaidika na mikopo hiyo mwaka 2003/04. Hapo awali, Serikali ilikuwa ikifaidika na misaada kutoka nje kupitia kwenye asilimia 4.5 ya ruzuku tu.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009/2010 Serikali inatarajia kupokea jumla ya TSh. 199,188 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya programu na miradi mbalimbali iliyopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2009/10. Mapato hayo ni sawa na asilimia 48.3 ya mapato yote. Kati ya fedha hizo, TSh. 96,879 milioni zitatokana na ruzuku na TSh. 102,309 milioni zitatokana na mikopo.

Matumizi kwa kazi za kawaida
Mhe. Spika, matumizi kwa kazi za kawaida kwa mwaka 2009/10 yanatarajia kufikia TSh. 172,692 milioni ambapo mishahara ya mawizara na taasisi za Serikali zinazopata ruzuku zimefikia TSh. 82,857 milioni sawa na asilimia 48 ya matumizi yote ya kazi za kawaida. Matumizi mengineyo kwa Mawizara na Taasisi pamoja na Mfuko Mkuu wa Serikali ni TSh. 89,835 milioni sawa na asilimia 52 ya matumizi yote ya kawaida.

Matumizi ya Fedha za Misaada ya Kibajeti 2009/10

Mhe. Spika, lengo kuu la misaada ya kibajeti ni kutekeleza mikakati ya kupunguza umaskini. Kwa hivyo, mgawanyo wa fedha hizo katika bajeti ya mwaka 2009/2010 umezingatia kipaumbele katika maeneo yafuatayo:

(i) Kuimarisha sekta ya Utalii kupitia Maendeleo ya Miundombinu; mkazo zaidi ukiwa katika kuimarisha viwanja vya ndege, barabara, kuimarisha Chuo cha Utalii, nishati na maji safi na salama. *(Makofi).*

(ii) Kuimarisha uwekezaji katika sekta ya kilimo kwa lengo la kuongeza uzalishaji kwa ajili ya masoko ya ndani na nje. Kuwa na uhakika wa chakula na kuongeza thamani kwa bidhaa zinazozalishwa kwa kushirikisha sekta binafsi na wajasiriamali wa kati na wadogo (SME).

(iii) Utekelezaji wa mpango mkuu wa umwagiliaji maji na uvuvi wa bahari kuu.

(iv) Kuimarisha huduma za afya ya jamii, mkazo zaidi ukiwa katika kuzuia vifo vya watoto wachanga na mama wajawazito.

(v) Kuimarisha huduma za elimu, mkazo ukiwa katika kujenga uwezo wa kitaasisi na watumishi.

(vi) Utekelezaji wa mageuzi ya msingi.

Mhe. Spika, matumizi ya kazi za maendeleo kwa programu na miradi kwa fedha za Washirika wa Maendeleo zinatarajiwa kufikia TSh. 199,188 milioni. Hivyo, jumla ya matumizi kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2009/2010 yanatarajiwa kufikia TSh. 412,605 milioni, sawa na ongezeko la asilimia 20.7 ya bajeti yote ya mwaka uliopita (2008/2009).

Muhtasari wa Mgawanyo wa Matumizi ya Serikali 2009/10

Mhe. Spika, mgawanyo kamili wa rasilimali kwa bajeti ya mwaka 2009/2010 baada ya kuzingatia rasilimali ziliopo ni kama ilivyo katika Kitabu cha Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo wa mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika, tukizingatia jumla ya mapato yote yanayotokana na vyanzo vya ndani na michango ya Washirika wa Maendeleo yanafikia TSh. 409,099 milioni na jumla ya matumizi ya TSh. 412,605 milioni. Hapo utaona kumejitokeza pengo la bajeti la TSh. 3,506 milioni (nakisi) ambalo

linategemewa kuzibwa kwa mikopo isiyokuwa ya kibenki *(treasury bills/bonds).*

Mhe. Spika, Serikali itaimarisha utaratibu wa uingizaji fedha katika maidara na taasisi zake kutoka katika mfuko mkuu wa serikali. Hatua hii tunategemea itaimarisha mfumo, taratibu na nidhamu za matumizi. Taratibu zitakazoandaliwa ni pamoja na mambo yafuatayo:

i) Maombi ya mahitaji ya fedha ya kila mwezi *(cash flow)* ya kila Wizara yatapaswa kuainishwa kwa uwazi kwa ajili ya kukidhi matumizi yatakayofanyika katika kila idara Unguja na Pemba.

ii) Maombi yatakayowasilishwa Serikalini kutoka katika kila Wizara yapate idhini ya Afisa Mhasibu *(Accounting Officer)* wa Wizara au taasisi husika.

iii) Serikali itatoa fedha kulingana na uwezo na maombi yaliyoidhinishwa na Afisa Mhasibu husika.

iv) Serikali itatoa taarifa ya kuwajulisha Afisa Mhasibu kila inapochukua hatua ya kuwaingizia fedha za matumizi katika vifungu vyao.

v) Fedha zinazohusiana na matumizi yatakayofanyika Pemba zitapelekwa moja kwa moja katika hesabu ziliopo Pemba. *(Makofi).*

JUHUDI ZA KUIMARISHA MAPATO

Mhe. Spika, kutokana na kukuwa kwa mahitaji ya matumizi ya Serikali, katika mwaka wa fedha 2009/10, Serikali imepanga kuchukua juhudi kubwa zaidi katika kuimarisha ukusanyaji na usimamizi wa mapato nchini. Hatua zinazopendekezwa kuchukuliwa ni pamoja na hizi zifuatazo:

(i) Kuanzisha kodi ya ardhi kwenye matumizi ya bahari yanayoambatana na ujenzi wa gati *(Jetty)* katika mahoteli ya kitalii. Kodi hii inalenga kupunguza ujenzi wa gati hizo ili kulinda mazingira.

(ii) Utayarishaji wa Sera ya Ukusanyaji na Usimamizi wa Mapato nchini.

(iii) Kuimarisha taratibu za ukusanyaji wa mapato yasiyotokana na vianzio vya kodi.

(iv) Kuanzishwa kwa Baraza la Ushauri la Walipa kodi.

(v) Kupunguzwa kwa kiwango cha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kutoka asilimia 20 hadi asilimia 18. Hatua hii inalenga kuhakikisha kuwa Zanzibar inabakia na uwezo wa kuhimili ushindani wa kiuchumi wakati huu ambapo

dunia imekumbwa na msukosuko wa fedha. Upungufu wa mapato unaokadiriwa kufikia TSh. 2,000 milioni kwa mwaka kutokana na kupunguzwa kwa kiwango cha kodi hii ya thamani yaani VAT unatarajiwa kufidiwa na mapato yanayotokana na kuimarika uwajibikaji wa hiari kwa upande wa wafanyabiashara.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza washirika wetu wa maendeleo kwa misaada yao wakiwa ni pamoja na wafuatao: BADEA, BELGIUM, UNDP, UNFPA, UNICEF, CARE AUSTRIA, DFID, WHO, JSDF, WSPA, WB, SIDA, IPEC, EGYPT, JAPAN, IDB, FINLAND, ADB, GEF, GAVI, ILO, OPEC, USAID, GLOBAL FUND, DANIDA, CIDA, NORAD, SWEDEN, NORWAY, CHINA, FAO, UNESCO, UNAIDS, OMAN, JUMUIYA YA AL-YOUSEIF, AFRICA CAPACITY BUILDING FOUNDATION, REPUBLIC OF KOREA, IAEA, UNIDO, EU, USA, JICA, GERMAN, IRELAND, INDIA, HOLLAND, IMF, IFAD, CUBA, UN HABITAT na UK na wote wengine ambao pengina nimewasahau hapa. *(Makofi).*

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwaomba washirika hao wa maendeleo kuendelea kutimiza wajibu wao wa kutusaidia na kuongeza misaada ya maendeleo kama tulivyokubaliana katika azimio la *Monterey*. Nasi kwa upande wetu, tutaendelea na wajibu wetu wa kutekeleza mikakati ya kupunguza umasikini na kukuza uchumi, mageuzi ya msingi na hatimae tuweze kufikia malengo ya milenia ifikapo mwaka 2015. Misaada yao hiyo katika hali hii ya misukosuko inahitajika zaidi ili tusitetereke katika kutekeleza mipango yetu ya maendeleo.

Mfumo wa Bajeti kwa Mujibu wa Uwezo Halisi kwa Mwaka 2009/2010
(TSh. Milioni)

MAELEZO	**Makadirio 2008/2009**	**Makadirio 2009/2010**	***Asilimia ya Bajeti ya 2009/10***
MAPATO			
A. MAPATO YA NDANI	**134,550**	**159,697**	*38.7*
i) Mapato ya Kodi	124,709	148,932	*36.1*
ii) Mapato yasiyo ya kodi	9,841	10,765	*2.6*
B. MISAADA YA KIBAJETI	**31,407**	**50,214**	*12.2*
i) 4.5% misaada ya kibajeti	23,407	50,214	*12.2*
ii) Misamaha ya Madeni (MDRI)	8,000	0	*0.0*
C. HATI FUNGATE (T/Bills)	2,000	3,506	*0.8*
D. RUZUKU/MIKOPO	**173,752**	**199,188**	*48.3*
i) Ruzuku ya miradi/programu	101,325	96,879	*23.5*
ii) Mikopo ya miradi/programu	72,427	102,309	*24.8*
JUMLA YA MAPATO	**341,709**	**412,605**	*100.0*
MATUMIZI			
E. MATUMIZI YA KAWAIDA	**149,435**	**172,692**	*41.9*
i) Mishahara (Wizara)	64,095	73,763	*17.9*
Mishahara ya Taasisi (Transfers)	6,426	9,094	*2.2*
ii) Matumizi mengineyo (Wizara)	32,358	38,942	*9.4*
Matumizi mengineyo (Transfers)	11,395	12,073	*2.9*
iii) Mfuko Mkuu wa Serikali (CFS)	35,161	38,820	*9.4*
F. MATUMIZI YA MAENDELEO	**192,274**	**239,913**	*58.1*
i) Mchango wa Serikali	18,522	40,725	*9.9*
ii) Mchango wa Wahisani	173,752	199,188	*48.3*
JUMLA YA MATUMIZI	**341,709**	**412,605**	*100.0*

Chanzo: Idara ya Ukuzaji Uchumi na Bajeti

HITIMISHO

Mhe. Spika, mkakati wa kunusuru uchumi uliotolewa na serikali unahitaji umahiri wa pamoja katika utekelezaji; hii ikiwa ni pamoja na kuwa na msimamo wa pamoja kuitangaza Zanzibar, ili ibakie katika ramani ya utalii na kuweza kuongeza mapato kwa lengo la kuendeleza miundombinu.

Aidha, Mkakati wa Kuimarisha Kilimo uliopitishwa na serikali unahitaji nguvu ya pamoja, ili Zanzibar iweze kujitosheleza kwa chakula, kulisha soko la utalii na kusafirisha bidhaa nchi za nje. Suala la uimarishaji wa Kilimo cha Umwagiliaji litapewa kipaumbele *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza awali, mwaka 2008/2009 ulikuwa na changamoto nyingi zikiwemo misukosuko ya soko la fedha, mfumko wa bei, upungufu wa chakula, mwenendo usiotabirika wa bei za mafuta, mabadiliko ya hali ya hewa na maradhi ambukizi duniani. Haya yote yamepelekea athari katika uchumi wetu. Tunafahamu kwamba taathira hazikuukumba uchumi tu, bali hata maendeleo ya wananchi mmoja mmoja.

Serikali inatambua uduni wa maslahi ya watumishi kwa kuzingatia hali halisi ya gharama za maisha. Itakumbukwa kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Amani Abeid Karume katika sherehe za kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani Mei Mosi 2009 aliagiza kuangaliwa uwezekano wa kuongeza kima cha chini cha mshahara. Katika kutekeleza agizo hilo, Serikali inaongeza kima chini cha mshahara kutoka TSh. 80,000 kufikia TSh. 100,000 kwa mwezi *(Makofi)*.

Hata hivyo, kiwango hicho kipya kitafikiwa kwa awamu mbili kuanzia Oktoba 2009 ambapo kima hicho kitapandishwa kwa TSh. 10,000 wakati serikali ikifanya mapitio ya muundo wa watumishi (*scheme of service*) kwa kada zake zote, kazi ambayo inatarajiwa kukamilika mwezi Disemba 2009.

Mhe. Spika, awamu ya pili ya nyongeza ya mshahara ya TSh. 10,000 itatolewa kuanzia Januari 2010 na itaenda sambamba na utekelezaji wa muundo huo mpya wa utumishi. Kama ambavyo serikali imekuwa ikiahidi, itaendelea na kufanya mapitio ya maslahi ya wafanyakazi wake kadiri hali ya uchumi itavyoruhusu.

Mhe. Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kazi kubwa na nzito ya kutayarisha na hatimae kuniwezesha kuwasilisha mapendekezo haya ya bajeti mbele ya Baraza lako tukufu kwa wakati.

Aidha nawashukuru Katibu Mkuu, Manaibu Makatibu Wakuu, Mhasibu Mkuu wa Serikali, Makamishna, Wakurugenzi, Afisa Mdhamini Wizara ya Fedha na Uchumi Pemba, watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi hasa watendaji wa Idara ya Ukuzaji Uchumi na Bajeti kwa mashirikiano, uwajibikaji wao mkubwa pamoja na mshikamano waliouonesha.

Vile vile nawashukuru watendaji wakuu na wafanyakazi wote wa wizara na idara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar waliochangia utayarishaji wa bajeti hii, yenye lengo la kuimarisha miundombinu. Shukurani za pekee nazituma kwa taasisi zisizo za kiserikali ikiwemo sekta binafsi kwa ushiriki wao, katika mchakato wa utayarishaji wa bajeti hii kupitia vikao vya MKUZA. Pia Baraza la Biashara la Zanzibar na Vikundi Kazi vya Mikakati ya Uimarishaji Mapato pamoja na mikutano mbali mbali ya utaribu wa misaada.

Mashirikiano haya ya pamoja, yatatupelekea kuitekeleza bajeti yetu ya maendeleo ya miundombinu kwa kuimarisha kilimo na utalii kuwa ya mafanikio. Ni matumaini yangu kuwa, tutashirikiana katika utekelezaji wa bajeti hii na zaidi katika matayarisho ya bajeti zinazokuja.

Mhe. Spika, baada ya kuwasilisha mapendekezo haya, naliomba Baraza lako tukufu lipokee, lijadili na hatimae liyapitishe mapendekezo juu ya matarajio ya ukuaji wa uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2009/10, ili yawe muongozo wa utekelezaji wa shughuli za serikali kwa mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika, kwa maelezo haya, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapendekeza mbele ya Baraza lako tukufu kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kukusanya jumla ya TSh. 412,605 milioni pamoja na matumizi ya TSh. 172,692 milioni kwa kazi za kawaida na TSh. 239,913 milioni kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja *(Makofi)*.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imeungwa mkono na ninakushukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha kwa uwasilishaji wa Hotuba hii ya Bajeti ya Serikali jioni hii.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuendelea na shughuli zetu kuna matangazo matatu. Kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha kwa uwasilishaji wa bajeti, pia ninawashukuru Waheshimiwa

Wajumbe kwa kuwa watulivu muda wote huo kwa kusikiliza hotuba hii iliyowasilishwa.

Katika Kikao hiki cha Bajeti kwa siku ya leo tuliwaalika wageni mbali mbali ili waje wasikilize Hotuba hii ya Bajeti na nimearifiwa kwamba miongoni mwa waliofika hapa yupo Waziri Kiongozi Mstaafu Mhe. Ramadhan Haji Faki, Mufti wa Zanzibar Sheikh Harith Khelef, pia Mhe. *Professor* Ibrahim Haroun Lipumba Mwenyekiti wa Chama cha CUF. Vile vile Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Manaibu Makatibu Wakuu wa Vyama tofauti vya Siasa, wapo Makatibu Wakuu pamoja na Manaibu wa Idara na Taasisi za Serikali.

Pamoja na hawa wapo Mabalozi Wadogo mbali mbali wakiwemo Balozi Mdogo wa India, Oman, Egypt, Mwakilishi Mkaazi wa UNDP, Mwakilishi wa Balozi Mdogo wa China, Balozi Mdogo wa Heshma wa Sweden, pia yupo Mwakilishi Mkaazi *UNICEF*, pia yupo *Officer* kutoka *UNFPA* pamoja na *Officer* kutoka *ILO*, bila ya kumsahau Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania Rajab Baraka *(Makofi)*.

Kwa kweli tuliwaalika wageni tunashukuru na wengine sikupata karatasi zao. Lakini kama alivyosema Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha kwenye hotuba yake ya bajeti kwamba hata viongozi mbali mbali wa Sekta Binafsi wamefika. Kwa hivyo, kama kuna wengine sikuwataja basi naomba radhi, lakini nawakaribisha nyote kwenye mkutano huu kama vile tulivyowaletea mwaliko na ninawashukuruni kwa kuhudhuria katika mkutano huu mkuu *(Makofi)*.

Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wageni wetu waalikwa wote baada ya shughuli hii kubwa ambayo kwa muda mrefu tumekuwa watulivu, tunao utamaduni kwamba tunapowaalika wageni ni vyema tukajumuika pamoja nje na Katibu wa Baraza la Wawakilishi ameniambia kwamba kuna maandalizi maalum.

Kwa hivyo, mara baada ya kuahirisha shughuli zetu hapa, ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wageni wetu wote tukusanyike nje kwa lengo la kubadilishana mawazo kabla ya kwenda nyumbani.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo, taratibu za Kanuni za Baraza chini ya Kanuni ya 92 (5) inaeleza kwamba nimtake Mhe. Waziri Kiongozi au Waziri mwengine, ili atoe hoja ya kutoa muda usiozidi siku mbili, kwa ajili ya kutoa nafasi ya kupitia Hotuba ya Bajeti ya Serikali vizuri na baadaye kujadiliwa rasmi.

KUAHIRISHWA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha (Kny: Mhe. Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwamba uliahirishe Baraza kabla ya wakati wake, ili Waheshimiwa Wajumbe wapate wasaa wa kuipitia hotuba hii na tukutane tena hapa siku ya Jumatatu tarehe 22/06/2009 saa 3:00 asubuhi. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri ya kuahirisha shughuli zetu kabla ya wakati wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naafiki.

(Saa 11:41 jioni Baraza liliahirishwa hadi tarehe 22/06/2009 saa 3:00 asubuhi)